IBADA YA KILA SIKU

TOLEO LA 1

Jan-Feb-Mac 2021

# Habari Njema

## KILA SIKU

**BURE**
HAKIUZWI
KITABU HIKI CHA IBADA KIMESHALIPIWA NA WASHIRIKA WETU ILI KISAMBAZWE BURE

KAMA VILE MAJI YA BARIDI KWA MTU MWENYE KIU, NDIVYO ILIVYO HABARI NJEMA ITOKAYO KATIKA NCHI YA MBALI. [MITHALI 25:25]

Uebert & BeBe
ANGEL

SPIRIT EMBASSY

TheGoodNewsChurch®

WITH UEBERT AND BEBE ANGEL

WWW.UEBERTANGEL.ORG | WWW.GOODNEWSWORLD.COM




## UEBERT & BEBE ANGEL

Wakiwa na miaka mingi ya huduma, Uebert na Bebe Angel ni waanzilishi na sauti ya uogozi katika kutangaza habari njema ya neema ya Mungu (Euaggelion) na unabii ulimwenguni kote.

kati yao ni waandishi bora wa vitabu vya Spiritual Warfare, Intimacy, Prayer Banks, Supernatural Power of the Believer n.k. Uebert na Bebe Angel ni wazungumzaji wanaotafutwa kimataifa na kama viongozi kidunia, wanatambulika kwa maono, kuleta mabadiliko na ujasiri. kama waanzilishi wa kanisa la Good News (Spirit Embassy), na wenye ofisi ya kinabii, wamegusa maisha ya mamilioni ulimwenguni kote kupitia shauku yao ya kuvuna nafsi kwa kuleta ufunuo wa habari njema ya neema ya Mungu (Euagelion).

# Heri ya mwaka mpya!



**Isaya 43:18-19**
**Msiyakumbuke mambo ya kwanza, wala msiyatafakari mambo ya zamani.**
**Tazama, nitatenda neno jipya; sasa litachipuka; je! Hamtalijua sasa? Nitafanya njia hata jangwani, na mito ya maji nyikani.**

Mwaka mpya umewasilishwa ukiwa na tumaini jipya, ndoto mpya na malengo mapya. Pamoja na hayo, tunao wakristo wengi ambao hawawezi kusonga mbele na kuachana na mambo ya kale.

Maandiko yetu ya leo yanatueleza kwamba tusikumbuke mambo ya kwanza, sahau yote! Watu wengine huangalia sana yale makosa yao ya zamani, maumivu na maamuzi mabaya na kuvibeba kutoka mwaka mmoja mpaka mwaka mwigine. Hii inakuwa kama mzunguko na unajikuta umekwama kwenye wakati uliopita badala ya kuishi kwenye wakati wa sasa.

Mruhusu Mungu afanye jambo jipya ndani yako kama alivyoahidi kwenye neno lake. Mpatie Mungu nafasi ya kufanya hivyo kwa kurekebisha kilichomo kwenye akili yako. Achilia mambo ya zamani na tengeneza nafasi kwaajili ya mambo mapya. Mafanikio ya wiki hizi 52 zinazofuata inategemea na vile utakavyopanga akili yako.

Tuanze upya, sawa sawa?

## UKIRI WA KINABII

**Huu ni mwaka wa watu wa kimungu. Nitafanya makuu katika mwaka huu. Ninatamka kufunguka kwa kurasa hii mpya ya maisha yangu katika jina la Yesu.**

**SOMO LA ZIADA**
Mhubili 7:10

# Kuwa muangalifu na unachoona.



**Isaya 43:18-19**
**Mathayo 6:22-23**
**Taa ya mwili ni jicho; basi jicho lako likiwa safi, mwili wako wote utakuwa na nuru.**
**Lakini jicho lako likiwa bovu, mwili wako wote utakuwa na giza. Basi ile nuru iliyomo ndani yako ikiwa giza; si giza hilo!**

Siku hizi kuna mambo mengi maovu yanayoonekana. Uovu kwenye televisheni, uovu kwenye simu za mkononi na karibia kila mahali kwenye mitaa yetu. Macho yetu hufanya kazi kubwa kuanzia muda tunaoamka mpaka pale tunaporudi kulala. Angali macho yetu yako wazi, tunaendelea kuchukuwa taarifa kuhusu ulimwengu uliotuzunguka.

Maandiko ya leo yanakuja kama angalizo juu ya kuchuja yale tunayoona. Tunaweza kuwa wabarikiwa tuliojawa na mwanga ama waliopotea na kujawa na jiza kutokana na kile tulichochagua kuona.

Yafundishe macho yako nidhamu ya kuona mambo ya kimungu.

Nilishawahi kukutana na mwanamume mmoja ambae alinieleza kwamba akiwa mtoto, kuna mtoto mwenzake alileta picha za uchi ambazo walitazama wakiwa shule. Anaeleza kwamba picha hizi zilimuingia ndani ya nafsi yake na alijikuta akiendelea kuangalia picha za uchi mpaka hata baada ya ndoa yake. Ilimchukuwa miaka mingi katika neno la Mungu kuachana na hiyo tabia.

Kuwa muangalifu sana na unachoona. Weka macho yako katika mambo ya kimungu. Kumbuka kwamba wewe ni wa kimungu!

## UKIRI WA KINABII

**Macho yangu yanamtazamia Kristo. Hakuna giza linaloweza kunizuia. Mimi ni mwenye nguvu ndani ya Bwana na itakuwa hivyo siku zote katika jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Zaburi 121:1



**2 Wakorintho 4:4**
**ambao ndani yao mungu wa dunia hii amepofusha fikira zao wasioamini, isiwazukie nuru ya injili ya utukufu wake Kristo aliye sura yake Mungu.**

Andiko letu la leo linatuonesha jambo ambalo wakristo wengi hukataa na kushindwa kukubaliana nalo hata leo. Adamu na Hawa walimpatia shetani mamlaka kule bustanini kwasababu walimpa lawama ya kile kilichotendeka. Shetani alikubali ile lawama kwasababu alielewa kwamba alikuwa anapata mamlaka kutoka kwa Adamu. Ametumia hayo mamlaka kuwapofisha wale ambao wamechagua kutokuamini.

Vita kati ya Mungu na shetani haikuwa juu ya nani ni mkuu, shetani aliumbwa na anafahamu kwamba hawezi kuwa mkuu. Vita inahusu ibada.

Neno la Mungu linasema saa inakuja amabayo wamuaduo watamuabudu katika roho na kweli kwani Mungu baba anatafuta ibada ya namna hiyo.

Mungu anapenda waabuduo halisi. Husikubali kupotezwa na starehe za ulimwengu huu na ukajikuta ukiziabudu bila wewe kujua. Chochote ambacho unakipa umakini zaidi ndicho amabacho unaabudu na ndivyo unavyoangukia kwenye mikono ya adui.

Husikubali!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mwabudu halisi wa Mungu baba! Sitoondolewa umakini wangu na vitu vya ulimwenguni. Moyo wangu umekaa kwake kikamilifu na ndivyo nitakavyokuwa siku zote katika jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Yohana 4:23-24

## Kimbia kutoka kwenye dhambi- kuzimu kupo



**Warumi 6:1-2**
**Tuseme nini basi? Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi? Hasha!...**

Watu wengi hudhania kwamba neema inatupa ruhusa ya kutenda dhambi. Huu ni uongo uliyopitiliza. Ruhusa hiyo ya kuishi maisha bora na kupuuzia neno sio ya kweli.

Neema inakupa nguvu ya kuacha kutenda dhambi. Hauachi kutenda dhambi kwa nguvu zako mwenyewe, ni yule Roho wa Bwana ndani yako ndiye anaekusaidia kuacha dhambi.

Hivyo basi, unakimbiaje kutoka dhambini?

Ni kwa kujikita katika neno. Hivyo ndivyo unavyokuwa katika neema. Ile hamu ya mambo mabaya iliyokuwepo ndani yako, inaondoka ghafla. Hii ni kweli ambayo lazima itendewe kazi, hasa hasa hizi nyakati za mwisho. Husianguke kwenye dhambi. Hii ndiyo sababu Mungu alisema tafakari neno lake mchana na usiku. Alifahamu kwamba hii ndiyo namna ya pekee neema inaweza kuongezeka ndani yako na kukufanya uache kutenda dhambi.

## UKIRI WA KINABII

**Nimelindwa ndani ya Yesu kupitia neno lake. Ninahesabika kuwa wake na kuzimu sio sehemu yangu, wala sio sehemu ya yeyote alienizunguka. Niko huru kutokana na dhambi kwasababu ya neema yake. Haleluya!**

**SOMO LA ZIADA**
Mathayo 24:12



**Yakobo 2:19**
**Wewe waamini ya kuwa Mungu ni mmoja; watenda vema. Mashetani nao waamini na kutetemeka.**

Ukweli ni huu, kuamini kwako hakuleti utofauti, hata mashetani nao huamini na kutetemeka. Wakristo wengine hawafiki kwenye hatua ya kutetemeka. Hawaheshimu kitu chochote cha ufalme ikiwemo maombi.

Umewahi kwenda kwenye ibada ya kinabii na ukalinganisha na ibada ya maombi? Tofauti ni kubwa sana. Watu hawapendi kuomba. Maombi ni kama shughuli ambayo Mungu amewalazimisha kufanya.

Naomba nikueleze jambo, kuamini hakubadilishi maisha yako, kitakachobadilisha maisha yako ni maombi yaliojaa imani. Maombi na wewe ni kitu kimoja. Maombi ni maisha yako.

Siongelei maombi ambayo unaomba ili uonekane na watu kwamba unaomba vizuri na kwa nguvu zote. Husifanye maombi yako kuwa sanaa, na wewe msanii. Kuna watu wanatumia muda wakiwa nyumbani kujifunza namna ya kunena kwa lugha ili waonekane waliobobea pale watakapoitwa kuomba mbele ya kanisa siku ya Jumapili. Haitakiwi kuwa hivi.

Kuwa makini na maombi kwani mafanikio ya maisha yako yanatokana nayo.

## UKIRI WA KINABII

**Nimebarikiwa kuishi maisha ya maombi. Maisha yangu ni matokeo ya maombi na mafanikio yangu ni matokeo ya hilo.**

**SOMO LA ZIADA**
1 Yohana 5:14



**Marko 8: 23-25**
**Akamshika mkono yule kipofu, akamchukua nje ya kijiji, akamtemea mate ya macho, akamwekea mikono yake, akamwuliza, Waona kitu? Akatazama juu, akasema, Naona watu kama miti, inakwenda. Ndipo akaweka tena mikono yake juu ya macho yake, naye akatazama sana; akawa mzima, akaona vyote waziwazi.**

Jambo la ajabu kwenye maandiko yetu ya leo ni pale ambapo kipofu alisema anaona watu kama miti. Ni kwamba unaweza kuona ama hauwezi kuona. Hii inatuonesha kwamba kuna kitu ndani yake hakikuamka kwa wakati. Macho yake ya nyama yalifunguka lakini mtazamo wake haukuwa umefunguka.

Mtazamo wake uliitaji uponyaji hata baada ya macho yake ya nyama kufunguka. Macho yako yanaweza kuwa wazi lakini bado ukakosa uwezo wa kuona vizuri. Kama nabii, nimeona hili mara nyingi sana ambapo naona kwamba jambo linaelekea kubaya lakini hakuna anayeona. Na hata baada ya kuwaeleza jambo baya lililopo mbele yao, bado wanashindwa kuona.

Namna nzuri ya kuponywa upofu ni kujikita katika neno. Unapojiweka ndani ya neno, unaruhusu mtazamo wako kuwa sahihi. Maono yako yanakuwa wazi. Mambo ambayo hayakueleweka hapo zamani, yanaanza kuwa wazi.

Jiweke kando kila baada ya muda ili upate muda na Mungu kupitia neno lake. Hicho ndicho watu wa kimungu hufanya. Yesu alimpeleka kipofu nje ya kijiji kwasababu alitambua kwamba kutakuwa na vikwazo vingi.

Chukuwa muda kujikita katika neno. Itaondoa kila aina ya upofu.

## UKIRI WA KINABII

**Macho yangu ya nyama na roho yamefunguka kuona sawa sawa. Sitokosa muelekeo na upofu umeondolewa kwenye maisha yangu. Ninaona maisha yangu yajayo katika kiwango cha HD na yanavutia katika jina la Yesu.**

**SOMO LA ZIADA**
2 Wakorintho 4:3-4



**IMwanzo 7:16**
**Na walioingia, waliingia mume na mke, wa kila kitu chenye mwili, kama vile alivyomwamuru Mungu; Bwana akamfungia.**

Nuhu alionekana mjinga alipokuwa anazungumzia mafuriko. Ilikuwa rahisi kuyaacha mambo kama yalivyokuwa, kwenda kwenye vilabu na kuishi bila kujali. Ulifika wakati amabapo Mungu alifunga milango na hakuna alieruhusiwa kuingia.

Biblia inasema kwamba kama zilivyokuwa siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa kwenye ujio wa mwana wa Adamu. Tumebakiza muda mchache mpaka kufika mwisho wa dunia. Siku ya kunyakuliwa inakuja, sasa nitauliza hili swali, JE, UKO TAYARI KWA UNYAKUO?

Kama jibu lako ni hapana, mrudie Kristo na ishi vyema. Kuna uharaka kwenye ulimwengu wa roho, mlango unakaribia kufungwa.

## UKIRI WA KINABII

**Nimebarikiwa kuwa kwenye nyakati hizi kwasababu nitafikia wengi na habari njema za Yesu Kristo. Wengi wataokoka kwasababu mimi ni mvuna nafsi, Mungu atukuzwe!**

**SOMO LA ZIADA**
Mathayo 24: 37-39

## Je, utasimama kwaajili ya Kristo?



**Isaya 43:18-19**
**Zaburi 2:2**
**Wafalme wa dunia wanajipanga, Na wakuu wanafanya shauri pamoja, Juu ya Bwana, Na juu ya masihi wake.**

Maandiko ya hapo juu yanatueleza kwamba wafalme na malkia, serikali na wale walio katika nguvu wanapanga mambo yaliyo kinyume na Kristo. Hili ni jambo muhimu. Wakristo wanapigana vita na hata kupigana wao kwa wao. Malumbano yamekuwa sehemu ya kawaida kwenye baadhi ya familia. Ulevi wa mitandao ya kijamii na tabia potofu imekuwa jambo la kawaida. Watumishi wa Mungu wanafanyika kuwa wajinga na wachekeshaji hutumia jambo hili kwenye sanaa yao. Ni kama utani lakini Mungu hafurahii.

Wakati umakini wetu upo kwenye mambo haya yasio na msingi, jiza linaongezeka. Kila mtu amepoteza umakini badala ya kuangalia mambo ambayo ni ya msingi zaidi hivi leo, kusimama kwaajili ya Kristo na ufalme wake. Kuna watu kwenye mamlaka ambao yanafanya mambo kinyume na kanisa lakini sisi tupo kama hatuelewi kinachoendelea.

Tunaishi kwenye nyakati za mwisho. Itakuwa ngumu zaidi kuwa mkristo na inabidi tujifunze kushirikiana sasa kuliko wakati wowote ule. Je, utasimama kwaajili ya mpendwa mwenzako? Je, utasimama kwaajili ya Kristo?

## UKIRI WA KINABII

**Ninafahamu mimi ni nani na ninaelewa kusudi langu. Ninasimama kwaajili ya Ukristo. Ninasimama kwaajili ya wakristo wenzangu. Ninayo mamlaka juu ya viongozi waovu kwenye taifa langu. Yesu atashinda. Injili itashinda katika jina la Yesu!**

### SOMO LA ZIADA
1 Petro 2:9



**Luka 24:47**
**na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu.**

Natamani ujifunze jambo la muhimu sana kutokana na maandiko yetu ya leo. Wakristo huchanganya kati ya kusamehewa dhambi na kuondolewa dhambi, haya mambo ni mawili tofauti.

Naomba nikushtue, Mungu hakutusamehe dhambi zetu, Yesu alizilipia. Sasa kabla hujachanganyikiwa, naomba nikuelezee. Wokovu haukuwa bure. Kulikuwa na gharama ya kulipa na Yesu alikuwa hiyo gharama. Alisurubiwa kwaajili yetu. Hatukupata adhabu tuliostahili kwasababu mtu aliingilia kati na kuadhibishwa badala yetu.

Tofauti yake ni hii, msamaha unaacha rekodi ya uovu hata baada ya muda mrefu kupita baada ya kutenda uovu huo. Maondoleo ni neno ‘aphesis’ lenye maana ya ‘msamaha wa dhambi kama vile haikuwahi kutendeka’. Ni kuondoa dhambi kikamilifu. Dhambi hazipo tena, na hiki ndicho tulichopata kutoka kwenye msalaba.

Furahia! Yesu alilipia gharama na kuondoa kumbukumbu yote.

## UKIRI WA KINABII

**Niko huru kutoka kwenye utumwa. Hakuna kumbukumbu ya uovu wangu wa kale. Mimi ni kurasa mpya na hakuna mizigo ya zamani inayonirudisha nyuma. Asante Bwana Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Zaburi 103:12



**Waebrania 5:12**
**Kwa maana, iwapasapo kuwa waalimu, (maana wakati mwingi umepita), mnahitaji kufundishwa na mtu mafundisho ya kwanza ya maneno ya Mungu; nanyi mmekuwa mnahitaji maziwa wala si chakula kigumu.**

Haya ni mameno yenye uzito yaliyotamkwa na Paulo. Fikiria kwamba Mungu anataka kila mtu ana esoma andiko hili kuwa mwalimu wa neno! Anasema kwamba pale unapoona kwamba umekuwa bora katika neno, mtu anatakiwa kukufundisha mafundisho ya kwanza. Pale ambapo ulitakiwa kupewa chakula kigumu, bado mnahitaji maziwa kama mtoto.

Ni wajibu wako kukuwa katika amri za Mungu. Kila mkristo anatakiwa kuwa mwalimu kwani kuna mafunzo mengi yaliyofunzwa na taarifa nyingi zipo tayari wakati wowote.

Walakini, hauwezi kusema kwamba wewe ni mtume mzuri, nabii mzuri, ama mkristo bora bila mafunzo ya kwanza. Hivyo, chukuwa muda kujifunza na kukuwa. Mfuatilie mtumishi wako na vuna vilivyo kutoka kwenye shamba lake. Wewe ni mwalimu wa kimungu aliye kwenye matengenezo!

## UKIRI WA KINABII

**Nimeumbwa kwenye msingi wa neno na siwezi kuyumbishwa. Nimebarikiwa kuwa mwalimu wa neno la Mungu na niliyetayari kusambaza habari njema ya neema ya Mungu.**

**SOMO LA ZIADA**
2 Timotheo 2:15



**1 Yohana 1:10**
**Tukisema kwamba hatukutenda dhambi, twamfanya Yeye kuwa mwongo wala neno lake halimo mwetu.**

Ujumbe uliopo kwenye hili andiko letu ni kwamba lazima tutambue udhaifu wetu mbele ya Mungu na kwamba bila yeye hakuna namna tunaweza kujirekebisha. Husipotambua udhaifu wako, basi haujatubu.

Hii haihusii kusema udhaifu wako kwenye mitandao ya jamii ili kuonesha kwamba umetubu dhambi zako, hapana. Wakristo wanapenda kutubu hadharani na wanaona kwamba hiyo ndiyo namna sahihi ya kutubu. Hapana, sio kweli. Neno hilohilo limetumika kwenye tumpokea Kristo lakini hata isipofanywa kwenye runinga, bado inafaa.

Ukishatambua kile ulichokosea mbele za Mungu, chukuwa neema iliyopo kwaajili yako, upendo wake na maondoleo ya dhambi. Hicho ndicho kinachofaa! Hilo ndilo kusudi la Kristo kuja na kufa kwaajili yetu.

## UKIRI WA KINABII

**Ninatambua makosa yangu mbele ya Mungu siku ya leo. Na pia, ninatambua kwamba bila yeye siwezi kufanya mambo peke yangu. Asante Bwana kwa rehema yako ambayo iko, na ninachukuwa rehema hiyo kwaajili yangu katika jina a Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Waebrania 4:16



**Mithali 6:31**
**Lakini akipatikana, atalipa mara saba; Atatoa mali yote ya nyumba yake.**

Watu wanatumia muda mwingi kumuomba Mungu kile ambacho shetani ameiba. Biblia inasema fumbua macho yako na ukachukuwe! Umempata mwizi, hivyo chukuwa alichoiba na hata zaidi!! Tazama ujasiri wa Paulo,

Matendo 16:35-37
Kulipopambauka makadhi wakawatuma wakubwa wa askari wakisema, Waacheni watu wale waende zao. Yule mlinzi wa gereza akamwarifu Paulo maneno haya akisema, Makadhi wametuma watu ili mfunguliwe; basi, sasa tokeni nje, enendeni zenu kwa amani. Paulo akawaambia, Wametupiga mbele ya watu wote bil kutuhukumu, na sisi tu Warumi, tena wametutupa gerezani; na sasa wanataka kututoa kwa siri? Sivyo, lakini na waje wenyewe wakatutoe.

Unaona hiyo, baada ya Paulo kuwekwa gerezani kimakosa, aliomba makadhi kuja kumtoa kama walivyompeleka gerezani. Huyu mwanaume alifahamu yeye ni nani. Alikuwa amempata mwizi na alitaka kumlipisha, haleluyah!

Chukuwa kilicho chako kwa nguvu! Simama kwa ujasiri na mwambie shetani arudishe furaha aliyoiba, amani aliyoiba, na pesa alizoiba ikiwa na FAIDA. Arudishe angalau mara saba.

Kila mara ulipoaibishwa kwenye umati wa watu utabarikiwa mara saba zaidi kwenye umati wa watu katika jina la Yesu!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mji husioweza kufichika. Baraka zangu zitakuwa wazi kwa wote kuona. Kila aibu ya hadharani inabadilika kuwa baraka ya hadharani, haleluyah!**

**SOMO LA ZIADA**
Mathayo 5:14

## Mungu anayetosha na hata zaidi ya kutosha.



**Mwanzo 28:3**
**Na Mungu Mwenyezi (El Shaddai), akubariki, akuzidishe, na kukuongeza, ili uwe mkutano wa makabila.**

Neno shaddai linamaana mwenye mati-ti mengi. Hii inamaanisha kwamba Mungu anavyo vyote tunavyohitaji. Anatosha na hata zaidi ya kutosha. Ukiangalia maziwa ya mama, yana virutubisho sahihi vya kumsaidia mtoto kukuwa. Mtoto anavyonyonya zaidi, ndivyo ambavyo maziwa yanatoka zaidi. Mtoto anapoacha kunyonya, maziwa nayo yanaanza kupotea.

Kama hivyo hivyo, Mungu anavyo vyote tuna-vyohitaji na ni zaidi ya mahitaji yetu sote. Hu-sipochukuwa baraka zako, basi zinabaki bila kuchukuliwa.

Kuwa na uhakika kwamba kukosa sio mpan-go wa Mungu juu yako. Ni makosa kuishi bila kuwa na mahitaji ya kutosha kila siku.

Dai kilicho chako hivi leo! Wewe ni wa kimun-gu na mtu wa kimungu hua hapati taabu. Unae Baba ambae anatosha na hata zaidi ya kutosha.

## UKIRI WA KINABII

**Baba yangu amekwisha kunipatia zaidi ya mahitaji yangu. Ninayo mahi-taji yangu yote bila kukosa chochote. Utukufu kwa Mungu!**

### SOMO LA ZIADA
2 Wakorintho 9:8



**Matendo ya mitume 4:31**
**Hata walipokwisha kumwomba Mungu, mahali pale walipokusanyika pakatikiswa, wote wakajaa Roho Mtakatifu, wakanena neno la Mungu kwa ujasiri.**

Kama kuna kosa ndani ya ukristo, ni hili hapa. Nimesikia mara nyingi sana wakristo wakiomba kupewa ujasiri.

Maandiko yetu ya leo yanatueleza kwamba roho mtakatifu anakupatia roho ya ujasiri pale unapompokea. Ujasiri ni moja ya mambo ya kwanza kabisa ambayo roho mtakatifu aliwapatia waamini walipokuwa wanasubiria. Hakuna haja ya kuombea ujasiri. Kama Roho wa Bwana yu ndani yako, hakuna haja ya kuombea ujasiri. Hauogopi chochote kwani hakuna cha kukuyumbisha.

Ujasiri wa kiungu unaharibu uongo na kusimama na kweli ya Mungu. Inazungumza kilicho cha haki bila kujali ubaya wa hali iliyopo. Wakristo wenye ujasiri wanaonesha uwepo wa Roho wa Mungu ndani yao.

Kuanzia leo, amka kwenye kweli ya Roho mtakatifu aliyoko ndani yako na akupaye ujasiri. Husiogope. Wewe ni wa kimungu na hausimami peke yako.

## UKIRI WA KINABII

**Ninasimama imara kwenye maagizo ya Kristo. Siyumbishwi na kile ninachoona kimenizunguka. Ninao ujazo wa Roho Mtakatifu ndani yangu, hivyo, siko peke yangu. Ninayo mbingu upande wangu kila mara. Mimi ni JASIRI!**

**SOMO LA ZIADA**
Zaburi 28:1



**Mathayo 18:15**
**Na ndugu yako akikukosa, enenda ukamwonye, wewe na yeye peke yenu; akikusikia, umempata nduguyo.**

Andiko la kinabii la leo ni rahisi sana. Linasema kwamba kama kuna tatizo kati yako na mkristo mwingine, nenda kaongee nae pembeni. Hakuna namna nyingine!

Kwa bahati mbaya, tuko kwenye enzi za mitandao ya kijamii ambayo imeleta tabia za tofauti kwa wakristo. Madada na makaka hugombana mtandaoni ili dunia nzima ione. Wakristo huonesha makosa ya wakristo wenzio ili kuelezea chuki zao. Mpaka wapenzi hurumbana kwenye hii mitandao. Hii tabia sio ya kibiblia kabisa.

Mathayo anasema wazi kabisa kwamba matatizo kati ya wana wa Mungu yanatakiwa kusuluhishwa sirini. Husiruhusu kazi ya Mungu kudharaurika kwa kutangaza madhaifu ya watu wengine. Ni vyema kama ukienda kwa huyo mtu kuzungumza naye ama kwa njia ya simu.

Jambo lolote litendalwo kweye roho ya upendo huzaa matunda. Kama wewe ni mkristo kweli, basi utatamani makosa ya huyo mtu yarekebishike. Kwa namna hiyo utakuwa umepata ndugu. Husisababishe maumivu ya zaidi kwenye mioyo yao kwa kuwasema hadharani.

Huo ndiyo ukristo wa matendo.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mlinzi wa ndugu yangu. Ninawachunga wale niliopewa na Mungu kama familia yangu kwenye ufalme. Nitatembea kwenye upendo na kukaa hivyo katika jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Wagalatia 6:1



**Matendo ya mitume 10:4**
**Akamtazama sana, akaogopa akasema, Kuna nini, Bwana? Akamwambia, Sala zako na sadaka zako zimefika juu na kuwa ukumbusho mbele za Mungu.**

Ulishawahi kuwaza ni jambo gani unaweza kufanya ili kumfanya Mungu atie umakini kwako? Hasahasa kwenye nyakati ambazo unahisi yuko mbali nawe. Ukweli ni kwamba amekwisha kutuma umakini wake wote. Anaishi ndani yetu. Amekwisha kutupa kilicho bora zaidi. Hilo limekwisha fanyika.

Ukiangalia upande mwingine, maandiko yetu ya leo yanatuonesha jambo kama kifaa kwenye utendaji kazi. Inaonekana kuna kitu unaweza kufanya ambacho kinaweza kusababisha mbingu yote kusimama na kukutazama wewe.

Corinelio alitoa sadaka ikawa ukumbusho mbele ya Bwana na akafanya mambo kufurahisha. Hilo neno 'ukumbusho' kwa kiyunani ni 'kumbukumbu ya mtu ama kitu iliyotunzwa kwa muda mrefu'. Ni kama kizuizi kilichojiinua mpaka mbinguni. Huyu mwanaume aliomba na kuchanganya maombi yake kwa sadaka ya kujitoa na itafanya mbingu kuona jambo hilo.

Unaweza kuomba na kutoa (kwa kufanya yote mawili kwa wakati mmoja), na ikawa kama kizuizi ambacho mbingu haiwezi kutokuona. Inakupa umakini wa Mungu kikamilifu na hata zaidi.

Weka utoaji kwenye maombi yako. Inatengeneza kumbukumbu yako ambayo Mungu hawezi kupuuzia!

## UKIRI WA KINABII

**Ninaweka sambamba utoaji wangu na maombi yangu. Maisha yangu yatainuka kama kumbukumbu ambayo haiwezi kupuuziwa. Nimebarikiwa na ninayo alama ya kudumu mbinguni katika jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Mathayo 26:7

OSBORN INSTITUTE of THEOLOGY



CERTIFICATE / DIPLOMA

**1ST SEMESTER STARTS**
**1 MARCH 2021**

# ENROLMENT NOW OPEN

THE OSBORN INSTITUTE OF THEOLOGY FOUNDED BY PROPHET UEBERT ANGEL AND FULLY ACCREDITED BY TRANSWORLD ACCREDITING COMMISSION INTERNATIONAL, PROVIDES AN AWARD-WINNING ONLINE LEARNING PLATFORM THAT EQUIPS MEN AND WOMEN WITH THE REVEALED WORD OF GOD. OIT PREPARES MEN AND WOMEN TO SHARE AND BEAR WITNESS OF JESUS CHRIST TO THE CHURCH AND THE WORLD.

ENROL NOW AT WWW.OSBORNINSTITUTE.COM


LEARN HOW TO BE A
MILLIONAIRE
MILLIONAIRE
ACADEMY
WITH UEBERT ANGEL
REGISTER NOW AT
WWW.THEMILLIONAIREACADEMY.ORG



**1 Yohana 1:9**
**Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.**

Watu wanapoona andiko hili, wanachokiwaza ni kutafuta ndugu wa kumueleza mambo yao machafu. Kumwambia mtu juu ya maisha yako ni makosa. Pamoja na kwamba jambo hili linakubalika sana ndani ya ukristo, liko mbali sana na ukweli! Niruhusu nikuoneshe maana sahihi ya neno kuungama.

Neno kuungama ni neno — HOMOLOGEOkunena sambamba na mtu mwingine, yaani kukubaliana na jambo fulani.

Hii inamaanisha kwamba kama nikisema sawasawa na kile ambacho Mungu anasema kuhusu dhambi zangu, nakuwa nimesamehewa. Hiyo ndio maana ya kuungama. Mungu anasema nini juu ya dhambi? — zimeondolewa. Haziko kwenye maisha yako tena. Haijalishi upo ndani ya dhambi kiasi gani, tayari umekwisha kuwekwa huru, umesafishwa kwa damu ya Yesu! Hii ni neema ndungu zangu, hii ni habari njema kwa wale wa kimungu!

Acha kujiuliza ni nani unatakiwa kumueleza mambo yako ya zamani. Nena hivi;

NIMESAMEHEWA — HIVYO NIKO HURU!

## UKIRI WA KINABII

**Mambo yote yasiyo ya haki ndani yangu yamesafishwa kupitia Kristo. Mimi sio yule wa zamani. Maisha yangu yanatoka kiwango kimoja cha neema hadi kiwango kingine. nimebarikiwa, Nimesamehewa na sijalaaniwa katika jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Waefeso 1:7



**Yakobo 1:2**
**Ndugu zangu, hesabuni ya kuwa ni furaha tupu, mkiangukia katika majaribu mbalimbali.**

Mwaka mpya umewasilishwa ukiwa na tumaini jipya, Neno 'hesabu' lililotumiwa na Yakobo kwenye andiko letu ni neno linalofurahisha sana katika uhasibu. Hili neno halina maana kwamba unatakiwa kuburudika unapopata taabu. Hakuwa na maana kwamba ukizidiaha na tatizo lako la kodi, biashara yako inayofeli na mahusiano yako mabaya, bado uwe na furaha, hapana.

Kuhesabu hapa inamaanisha kwamba, yapime yale yote unayopitia na fahamu kwamba utafaulu mwisho wa siku. Yapime haya mambo na tambua kwamba Mungu ni mkuu kuzidi yote. Yapima na tambua kwamba jina lake ni kuu kuliko majina ya hayo mambo. Hesabuni ya kuwa ni furaha kwasababu hakuna jambo kuu kumshinda Mungu, haleluya!

Zingatia kwamba maandiko hapo juu yanaonesha wazi kwamba majaribu yatamkuta mkristo. Hivyo hisikushtue, jua kwamba majaribu yatatokea na utaweza kusonga mbele. Husiruhusu hili kuua ndoto zako kwani furaha ni uamuzi wako na sio hisia.

Hesabuni ya kuwa ni furaha tupu! Utakuwa bora zaidi na sio mwenye maumivu zaidi.

## UKIRI WA KINABII

**Roho yangu inabubujikwa na furaha. Siyumbushwi na majaribu kwani nimeyapima na kugundua kwamba Mungu ni mkuu kushinda yote. Ninahesabu yakuwa ni furaha tupu, haleluya!**

**SOMO LA ZIADA**
Warumi 15:13



**Waamuzi 16:15,17**
**Mwanamke akamwambia, Wawezaje kusema, Nakupenda; na moyo wako haupo pamoja nami? Umenidhihaki mara hizi tatu, wala hukuniambia asili ya nguvu zako nyingi. Ndipo alipomwambia yote yaliyokuwa moyoni mwake...**

Wengi wanaweza kumtazama Samson na kuona kwamba ni mjinga kwa kuanguka kwenye mitego ya Delila. Kitu ambacho haufahamu ni kwamba hata wewe hivi leo unae Delila wako, anaweza kuwa rafiki, mfanyakazi mwenzako au hata mwenza wako. Watu wengi wanatabia ya kuruhusu mahusiano mabovu wakitambua kabisa matokeo yake ambayo sio mazuri.

Kupitia urafiki aliokuwa nao na Delila, Samsoni alipoteza kile ambacho Mungu alimpatia. Alianguka kwasababu ya mtu mmoja tuu aliyemruhusu kumwingilia kwenye maisha yake. Delila alikuwa wa kwanza kupiga kelele kwamba Wafilisti wanakuja, pamoja na kwamba ni yeye ambaye aliwapa taarifa.

Tumia hekima sana kwenye swala la marafiki zako. Badilisha mawasiliano yako, hasahasa mwaka huu mpya. Anza maisha kwenye kurasa mpya na waondoe watu kama Delila. Baraka yako ya mtu wa kimungu inategemea uamuzi huu.

## UKIRI WA KINABII

**Ninajiondoa na kujitoa kutoka kwa watu wabaya maishani mwangu. Naondoa mahusiano yeyote ambayo ni sumu kwangu katika jina la Yesu. Baraka yangu ni ya uhakika. Upako wangu ni wa hakika, haleluya!**

### SOMO LA ZIADA

1 Wakorintho 15:33, Muhubiri 13:20



**Waebrania 12:1**
**basi na sisi pia, kwa kuwa tunazungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi; na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu,**

Saa ya kiroho inasonta katika wakati wa mwisho kabisa tulionao kwenye ulimwengu, tuko kwenye nyakati za mwisho. Kwa kufahamu hili, kizazi chetu kinatakiwa kubadilika na kuanza kuongozwa kwa nguvu kamilifu ya roho mtakatifu.

Kwenye mbio za kijiti, mtu wa kwanza anakuwaga mwenye uwezo mkubwa wa kukimbia. Mkimbiaji huyu anatakiwa kufanya vizuri ili kusaidia wale wanaokuja baada yake kukuta ushindani kwenye sehemu nzuri. Mtu wa mwisho ni wa muhimu sana pia kwasababu ndiye anaeleta ushindi. Ikitokea kwamba aliyeanza alikuwa taratibu, basi wa mwisho lazima akazane ili wapate ushindi.

Sisi ndio wamalizaji wa mbio hizi. Mitume walianza vizuri baada ya ufufuko wa Kristo, na sasa ni juu yetu kumaliza vizuri! Tutatenda makuu kuzidi chochote ambacho yeyote amewahi kuona-- SISI NI WA KIMUNGU!!

## UKIRI WA KINABII

**Ninejiandaa kwaajili ya kusukuma sehemu ya mwisho ya ukristo. Niko tayari kumaliza hizi mbio kwa nguvu na sitoangalia nyuma. Mbele daima, nyuma tena hakuna!**

**SOMO LA ZIADA**
1 Wakorintho 9:24-27



**Mathayo 12:36-37**
**Basi, nawaambia, kila neno lisilo maana, watakalolinena wanadamu, watatoa hesabu ya neno hilo siku ya hukumu. Kwa kuwa kwa maneno yako utahesabiwa haki, na kwa maneno yako utahukumiwa.**

Watafiti husema kwamba mtu wa kawaida huzungumza kati ya maneno 7000 mpaka 30000 kwa siku na wapo waliobobea wanaozungumza zaidi ya hayo.

Katika maandiko yetu ya leo, biblia inasema kwamba kila neno lisilo maana, watakaonena wanadamu, watatoa hesabu ya neno hilo siku ya hukumu. kuna wazo la kusikitisha mahali hapa. Nafahamu wengi wenu mmekwisha kuanza kufikiria mambo mengi ambayo mnenayo ambayo sio ya maana.

Maneno yenu yana maana sana. Yakiwa hasi ama chanya, yanao uwezo wa kutengeneza mizizi. Biblia inasema kwamba kwa maneno yako utahesabiwa haki na kwa maneno yako utahukumiwa. Umepewa nafasi ya kuchagua upande unaotaka.

Husiwe mkristo ambae anazungumza juu ya kila jambo. Ipo siku utatakiwa kuelezea hayo mambo. Kuwa na hekima. Tumia muda wako mwingi kujadili mambo ambayo yatakujenga wewe pamoja na wengine, na sio mambo ya kuharibu.

## UKIRI WA KINABII

**Maneno yangu yamewekwa mahali sahihi. Sitozungumza meneno yasio haki ambayo hayatonijenga mimi na wale walionizunguka. Ninasababisha mabadiliko kwa maneno yangu yaliojaa imani sasa hivi katika jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
1 Yakobo 3:10



**Isaya 9:6**
**Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, Tumepewa mtoto mwanamume; Na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake; Naye ataitwa jina lake, Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani.**

Tazama ambavyo hii ni namna nzuri ya kumueleza Baba yetu. Maelezo yaliyotoshelea, haleluya!

Nataka kuingia ndani zaidi kwenye maneno 'ajabu' na 'mshauri' yaliyotumika kwenye maandiko yetu ya leo. Haya maneno mawili kwa kiyunani yana maana hii;
Ajabu-- chenye nguvu, kisicho kawaida.
Mshauri-- mpanga mikakati

Tukiwa na hizi maana, tunaona maandiko yakipata maumbile mapya. Mungu sio wa ajabu pakee, ni mshauri wa ajabu, mpanga mikakati wa ajabu, haleluya! Anajua namna ya kupita kwenye kila hali. Ni mfunzi mzuri kwani yeye ndiye njia. Yeye ni mwanga hivyo siwezi kupotea gizani. Hata maisha yetu ni yeye!

Kuanzia leo husiyumbe unapopitia majaribu. Kumbuka kwamba ulionaye sio mpanga mikakati tuu, unaye mpanga mikakati wa ajabu. Ni wa tofauti katika mambo yake yote hivyo ni lazima ufaulu.

## UKIRI WA KINABII

**Ninaye mpanga mikakati wa ajabu, ninaye mshauri wa ajabu upande wangu. Nitashindwa vipi? Kushindwa sio sehemu yangu. Nimefanikiwa na siombi msamaha juu ya hilo, haleluyah!**

**SOMO LA ZIADA**
Joshua 1:9



**Waefeso 3:10**
**Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu;**

Tafakari kazi ya mjenzi. Anaketi na vifaa vyake na kuanza kuchora kile kilichomo kwenye akili yake. Anaelezea kile anachoona ndani yake kwa kukichora kwenye karatasi. Anachora mpaka vile vilivyomo ndani ya nyumba, vyumba, jiko, na hata eneo la kufuga kama mtu atapenda kufuga. Ni ndoto zake zikiwa zimepewa uhai.

Wewe ni mjenzi wa maisha yako. Unaweza kuamua utakuwa nani. Utakapofikia na hali yako ya kiroho ni juu yako. Kiasi gani kitakuwa kwenye akaunti yako ya benki ni juu yako. Amani yako, furaha yako ni juu yako. Maandiko ya leo yanasema ipo nguvu ndani yetu ya kusababisha haya mabadiliko.

Anza kuyachora maisha yako kwa maneno yako na namna unavyojibeba. Ona mafanikio yako kwenye macho ya akili yako. Ona kila kitu kama vile ufikiriavyo, inakuwa rahisi kufanyika kweli.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mjenzi wa maisha yangu. Ninaamua yaliyo bora tu kwenye maisha yangu. Ninatamka maisha ya mafanikio. Ninatamka maisha ya utele katika jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
2 Petro 1:3



**1 Petro 5:7**
**huku mkimtwika yeye fadhaa zenu zote…**

Gari moshi linapoingia kwenye handaki, hauwezi kutupa ile tiketi yako na kuruka kutoka kwenye gari moshi, bali unakaa na kumuamini mhandisi.

Kumuamini Mungu ndivyo ilivyo. Kuna wakati unapitia kwenye andaki na inaonekana kana kwamba suluhisho ni kuchukua hatua mikononi mwako. Ni chaguo lako kuwa na imani hata kama mambo yote yaliyo kuzunguka yanaenda kinyume nawe.

Maandiko yetu ya leo yanasema kwamba 'huku mkimtwika yeye fadhaa zenu zote', neno kutwika inamaanisha kurushia. Inamaanisha kwamba unarusha kila kitu ulichonacho kwa Yesu. hautaki uwe kwenye giza kwani anakujali sana na anasubiria umrushie mizigo yako.

Yeye ndio muhandisi na anataka vitu bora kwaajili yako. Hivyo, muamini. Hata kwenye hali mbaya ya maisha yako.

## UKIRI WA KINABII

**Siogopi vitu vigumu kwani najua kwamba siko peke yangu. Ninamrushia Yesu kila mzigo niliokuwa nimebeba. Niko kwenye mikono salama na itakuwa hivyo siku zote, Mungu atukuzwe!**

**SOMO LA ZIADA**
Marko 14: 34-36



**2 Timothy 3:4**
**wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu;**

Kwenye andiko letu la leo, mtume Paulo ametumia neno Philadonos- lenye maana ya 'wapenda anasa'. Alikuwa anamaana kwamba watu kwenye siku ya mwisho watakuwa wapenda anasa.

Inasikitisha kutambua ya kwamba, kwenye hizi siku za mwisho hata wakristo wamekuwa wapenda anasa na faraja kiasi kwamaba hawataki kuombwa kufanya jambo lolote ambalo litawapa usumbufu. Hata kuwaalika watu kanisani ni ngumu kwao. Wachungaji wanaogopa kuwaonya wahumini juu ya tabia mbovu kwani kumuonya muumini ni kumpoteza.

Kuwa mwangalifu usiendeshwe na anasa zako mpaka ukajikuta kwenye mikono ya adui. Hisia hupotea na ndo maana Mungu anatufundisha kuweka umakini wetu katika utii na sio anasa.

Hivi karibuni kila kitu cha ulimwengu huu kitapita na ni vile vitu vya Yesu tuu ndio vitakavyo baki. Utazame moyo wako kutambua hali yako ya kiroho. Kama kuna maeneo yanayohitaji kurekebishwa, muombe Roho wa Mungu akurekebishe kadri unavyokuwa katika neno.

## UKIRI WA KINABII

**Ninachagua kumuabudu Mungu na kukaa katika neno. Anasa za ulimwengu huu sio sehemu yangu, mali zangu za kweli zinawekwa mbinguni ambapo hazitoweza kupotea. Tumsifu Mungu!**

**SOMO LA ZIADA**
1 Yohana 2:15



**Yohana 16:23**
**...Ulimwenguni mnayo dhiki lakini jipeni moyo mimeushinda ulimwengu.**

Huu ni uhakikisho wa kipekee kutoka kwa Yesu. tafakari juu ya hili kwa mara moja. Haijalishi ni changamoto gani tutapitia kwenye siku za usoni, Yesu amekwisha kutamka nafasi yetu ya imani, 'jipeni moyo' kwani amekwisha kushinda yote. Hizi ni faida za wana wa kimungu.

Kwa kiyunani neno changamoto ni neno thlipsis ambalo linaelezea dhiki, taabu na changamoto ambayo ni nzito sana. Yesu alinena kwamba ameyashinda haya yote. Kwa kupitia hili neno, Yesu alieleza kwamba mambo hayatokuwa rahisi sana kwa wale watakaochangua kumfuata. Pamoja na hayo, lolote ambalo litarushwa kwako kutoka kwenye ulimwengu, Yesu alikwisha kunena na bado ananena hata hivi leo, 'jipeni moyo, nimeushinda ulimwengu.'

Hivyo basi, badala ya kumruhusu shetani kukusumbua kwa mawazo kwamba hakuna tumaini ama hauwezi kushinda changamoto zinazokujia kutoka kila pande, ushikilie ukweli na kwamba unatoka kwenye hii hali ngumu kwa kushangilia!

## UKIRI WA KINABII

**Moyo wangu umejawa na furaha kwasababu ninaelewa uhakika wa Kristo. Nimekwisha ushinda ulimwengu kupitia yeye. Hakuna cha kuogopa katika jina la Yesu! NINAJIPA MOYO!**

### SOMO LA ZIADA
Yoshua 1:9



**Mathayo 10:16**
**...Basi iweni na busara kama nyoka.**

Kwa kuangalia haraka, maneno haya yanaweza kumshangaza hata mkristo bora. Lakini kama ukiyasoma maandiko vizuri, ukungu unaondoka na maagizo aliyotoa Kristo yanaeleweka. Tuangalie kutoka mwanzo.

'Anagalieni, mimi nawatuma kama kondoo kati ya mbwa mwitu basi iweni na busara kama nyoka, na kuwa wapole kama hua'

Neno 'nyoka' mahali hapa limetumika kama ishara ya ujanja ama hekima. Wakristo wengi wanalinganisha nyoka na uovu. Wanashtuka hata katika wazo la nyoka. Ambacho Yesu alikuwa anasema ni kwamba, nyoka wana hekima na tunatakiwa kujifunza kutoka kwao hasahasa katika wakati huu ambapo wakristo tunatakiwa kuwa makini na mazingira yetu.

Tazama, nyoka wameumbwa na uwezo wa kupotea wanapoingia kwenye mazingira, hasa hasa wanapoingia kwenye mazingira mapya. Wanajua jinsi ya kujificha na kusoma taratibu namna ya kupata chakula chao kirahisi. Wanakaa kimya na kutenda kwenye muda sahihi.

huu msemo unatuhusu sisi sote katika familia, biahara na fursa yeyote ambayo Mungu ametuwekea mbele yetu ili kufanikiwa hapa ulimwenguni.

## UKIRI WA KINABII

**Sikupewa akili ya woga. Nina busara kama ya nyoka. Ninajua ni wakati gani wa kukaa kimya, na wakati gani wa kutenda kwa kuongozwa na Roho mtakatifu, haleluya!**

**SOMO LA ZIADA**
Muhubiri 4:6-7



**Yakobo 1:27**
**Dini iliyo safi, hisiyo na taka mbele za Mungu Baba ni hii, kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhikiyao, na kujilinda na dunia pasipo mawaa.**

Andiko letu la leo ni jambo unaloweza kutendea kazi sasa hivi.

Kama wakristo, tunao jukumu la kuwasaidia wale wenye mahitaji kama yatima na wajane wanaohangaika baada ya kupoteza wenzi wao. Ni jambo jema na linalokubalika mbele ya Mungu kwa sisi kuwatembelea wajane katika hali hii.

Wajane wengi hupata shida nyingi kifedha na kimaisha pale mwenzi wake anapofariki. Mungu anatuomba kufanya kadri ya uwezo wetu ili kuwafariji katika wakati wao wa mahangaiko. Kwavile hii ni amri ya Mungu kama amri zake nyingine, naomba nikuulize; umefanya nini kwaajilii ya wajane?

Kama Good news World (Ulimwengu wa habari njema), tumebarikiwa na washirika ulimwenguni kote wanaotusaidia kuwa msaada kwa wajane. Nakutia moyo kufanya hata zaidi mwaka huu, mfikie mjane ambae ni jirani yako, mfanyakazi mwenzako na hata kanisani. Wanunulie mahitaji muhimu, wasaidie kifedha na kama msaada sio wa kifedha, tumia muda wako kwao. Jitolee hata kusafisha mazingira ya nyumba zao ili wahisi upendo wa Kristo kupitia wewe.

Wale wenye mahitaji ni jukumu letu. Tufanye hata zaidi!

## UKIRI WA KINABII

**Nina asili ya upendo. Upendo wa Mungu umenyunyizwa ndani ya moyo wangu. Ninafurahia kuchukuwa jukumu la kuangalia wale wenye mahitaji. Wataujua upendo wa Kristo kupitia mimi katika jina la Yesu.**

**SOMO LA ZIADA**
Muhubiri 19:7



**Wafilipi 3:13**
**Ndugu, sijidhanii nafsi yangu kwamba nimekwisha kushika ila natenda neno moja tu nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele.**

Huu ni mwaka mpya na ni wakati wa kutarajia baraka nyingi mpya. Inasikitisha, wakristo wengi wameanza mwaka huu wakiwa na msongo wa mawazo. Wanakumbuka ahadi zote walizowapa watu ambazo hawakuzitimiza, ama malengo walioshindwa kufikia. Wengine wanajilaumu kwa kushindwa kufikia hatua fulani kiroho.

Kupitia mtume Paulo, Mungu analo jambo la kusema kuhusu hili. Badala ya kuishi katika hali ya kujilaumu na kujionea huruma, tumia muda wako pamoja na Mungu. Yatubu makosa yako na mambo ambayo hukufanya uliotakiwa kufanya.

Ni wakati wako kuachilia mambo ya nyuma. Yapuuzie mambo ya zamani kwa maksudi. Ya kale yamekwisha pita, kwanini bado unayatazamia? Kwavile Mungu amekusamehe, acha kutazama nyuma. Huu ndio ukweli, unaweza kuweka ya kale nyuma na kutazama mbele.

Mungu amekupa zawadi ya mwaka mpya. Mwaka wa wakimungu, huu ni mwaka wako! Husitumie mwaka wako kwa mambo ya kale.

## UKIRI WA KINABII

**Mambo ya kale hayana nafasi sasa na siku zangu za usoni. Mimi ni kiumbe kipya ndani ya Kristo. Ninao ukurasa upya na sitotazama nyuma tena katika jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
2 Wakorintho 5:17



**Warumi 1:16**
**Kwa maana sionei haya injili kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia.**

Umekwisha kufika kwenye hatua ambayo unataniwa kwasababu ya imani yako? Sio jambo la kufurahisha kabisa lakini kama umepitia haya mashtaka, hauko peke yako, wewe sio wa kwanza wala wa mwisho.

Mtume Paulo alipata mashtak kwenye ulimwengu wa wapagani na wa ulimwengu wa wayahudi. Kuna wakati ambapo haikuwa maneno mabovu tuu aliyoambiwa bali aliteswa mwilini mwake na kupelekwa jela na wale watu waliokuwa na chuki juu yake. Bado aliweza kuangalia nyuma na kutamka 'SIIONEI HAYA INJILI YA MUNGU'

Husikate tamaa unapopoteza familia, marafiki ama wafuasi kwaajili ya imani yako. Husionee aibu Roho mtakatifu aliyeko ndani yako. Wewe ni nyumba ya nguvu inayotembea kwasababu ya Roho Mtaatifu. Hukufeli ulipochagua kumpenda bali ni tofauti kabisa na hilo.

Kuwa na furaha kama hakuna mtu wa kusikia. Tumia imani yako na uruhusu Mungu akutie nguvu juu ya chochote unachopitia sasa.

## UKIRI WA KINABII

**Sichanganyikiwi wala kuumia moyo pale ambapo watu wanaitania imani yangu. Sirudi nyuma kwasababu ya vitisho. Aliyeko ndani yangu ni mkuu kuliko aliyeko ulimwenguni. SIONI HAYA!!**

**SOMO LA ZIADA**
Isaya 50:7



**Waefeso 4:29**
**Neno lolote lililo ovu lisitoke vinywani mwenu, bali lililo jema la kumfaa mwenye kuhitaji, ili lipewe neema wanaosikia.**

Katika miaka yangu ya huduma nimeona yote, na katika hayo nimeona wakristo wakitenda mabaya, umbeya wao ni mbaya kuliko wote.

Angalia andiko letu la leo. Neno 'ovu' kwenye kigiliki ni neno ni 'sapros' lenye maana ya kuchacha ama kuoza. Neno kuchacha ni kuharibika na kutoa harufu mbaya. Umeshawahi kunusa nyama iliyooza? Inanuka vibaya sana. Hili ndilo neno alilotumia kuelezea maagizo haya.

Roho Mtakatifu anakuomba ufanyike furaha unapoongea na watu wengine na kuhusu watu wengine. Badala ya kuwa na matokeo maovu ya wambea kwa watu wao, jitahidi umwache mtu kwenye hali nzuri zaidi.

Fanya maamuzi kuanzia leo kwamba unapoondoka kwenye mazungumzo ama chumba, uache manukato bora ya Kristo. Waruhusu watu wakukumbuke kwa maneno yako mema uliyowaacha nao. Ruhusu watu wamalize mazungumzo nawe kwenye simu wakiwa bora kuliko walivyoanza.

## UKIRI WA KINABII

**Kuanzia leo mdomo wangu utanena mazuri tuu kuhusu watu wengine. Siongei umbeya juu ya watu wengine wala siwarudishi nyuma kwa maneno yangu. Ninaacha manukato bora ya Kristo kwa wale walionizunguka. Nimebarikiwa!**


**SOMO LA ZIADA**
Waefeso 4:29


Best Selling author of INTIMACY
BeBe Angel
Grace Driven Life
Proven Steps to Living a Guilt Free Life
GET YOUR COPY NOW!
BeBe Angel
Grace Driven Life
Proven Steps to Living a Guilt Free Life
www.uebertangel.org | www.bebeangel.org

Uebert angel (Major)

# GENETICS OF WORDS

#1 Best Seller




INTERNATIONAL BESTSELLING amazon AUTHOR

RECREATING YOUR WORLD THROUGH THE
SUPERNATURAL POWER BEHIND YOUR WORDS

**AVAILABLE TO ORDER ON**
WWW.UEBERTANGEL.ORG



**Wagalatia 3:29**
**Na kama ninyi ni wa Kristo, basi mmekuwa uzao wa Ibrahimu, na warithi sawasawa na ahadi.**

Sasa ambavyo umezaliwa upya, umekuwa uzao wa Ibrahimu na mrithi wa baraka za Ibrahimu. Napenda vile ambavyo biblia ya toleo la New Living inavyosema kwa kiingereza, 'ambavyo sasa sisi ni wa Yesu, tumefanyika kizazi cha Ibrahimu, na ahadi zote alizopewa ni za kwetu.' ushirika wako na Kristo umekufanya kuwa kwenye kizazi ya Ibrahimu, na kwasababu hiyo, baraka alizopewa na Mungu zimekuwa zako.

Kama mzawa wa Ibrahimu, hakuna jambo zuri sana kukuzidi. Umebarikiwa kupita kipimo. Kufeli, magonjwa, kukosa na kifo haviendani na maisha yako tena. Haiwezekani ukafeli ama kuwa masikini kwenye maisha yako kwasababu kama kizazi cha Ibrahimu, kazi za mikono yako zimebarikiwa. Umetawazwa kwaajili ya mafanikio. Kuzaa matunda ni haki uliozaliwa nayo. Huu ni urithi wako kama kizazi cha Ibrahimu.

Biblia inatuambia hadithi ya mwanamke ambaye alikuwa na ulemavu kwa miaka 18. Yesu alipomuona hekaluni alisema, 'na huyu mwanamke, aliye uzao wa Ibrahimu, ambaye shetani amemfunga miaka kumi na minane hii, haikupasa afunguliwe kifungo hiki siku ya sabato? (Luka 13:16) Alipokwisha kunena haya, alimgusa mgongoni mwake na kusema, 'mama, umefunguliwa katika udhaifu wako.'(Luka 13:12). Alipona hapo hapo. Kwanini? Kwasababu mbegu ya Ibrahimu haitakiwi kuteswa na magonjwa ama udhaifu.

Kama unasoma hii na umekuwa ukisumbuliwa na magonjwa ama udhaifu, tambua ya kwamba wewe ni mzawa wa Ibrahimu, hivyo hautakiwi kufungwa na kiharusi, upofu, ukiziwi, ulemavu, umasikini ama aina yeyote ile ya udhaifu.

## UKIRI WA KINABII

**Ninafanikiwa na ninaishi kwenye timilizo la baraka zako zisizoweza kupimika kwasababu mimi ni mzawa wa Ibrahimu. Mimi ni mrithi kulingana na ahadi na mrithi pamoja na Kristo, nimebarikiwa mjini, nimebarikiwa mashambani, nimebarikiwa kutoka kwangu na kuingia kwangu! Nimebarikiwa kuwa baraka!**

**SOMO LA ZIADA**
Luka 13:16



**1 Petro 2:9**
**Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie nuru yake ya ajabu.**

Mwanadamu alipoteza haki yake juu ya ulimwengu alipotenda kosa na kumpatia shetani mamlaka. Baadae Yesu alikuja, akafa, akaenda kuzimu kumshinda shetani na kuchukuwa hayo mamlaka kutoka kwa shetani (wakolosai 2:15). Hata baada ya hayo, alifufuka kutoka wafu na kupaa mbinguni.

Bwana Yesu alitupa mamlaka ya kifalme. Unapozaliwa upya, unazaliwa mfalme. Wewe ni sehemu ya familia ya kifalme inayotawala ulimwengu. Ndio maana Petro anasema kwamba 'ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie nuru yake ya ajabu.'

Wafalme huzaa wafalme na mabwana huzaa mabwana. Umezaliwa na Mungu, hivyo wewe ni mfalme na sio mtu wa kawaida. Wewe sio wa masikini, wewe ni wa kimungu. Tambua urithi wako. Tembea ndani ya uelewa huu. Tumia fursa ya kuwa mtumishi wa kifalme kama mwamini. Wafalme hutawala, hivyo tawala maishani kama mfalme na shetani na wafuasi wake wataenenda kulingana na matamshi yako.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni wa kifalme, mimi ni mtoto wa mfalme. Nakataa kuwa masikini, utajiri ni urithi wangu katika jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Ufunuo wa Yohana 1:6



**Yohana 6:63**
**Roho ndiyo itiayo uzima, mwili haufai kitu maneno hayo niliyowaambia ni roho, tena ni uzima.**

Kila neno ambalo umewahi kunena liko hai sehemu fulani kwenye ulimwengu wa roho, halijafa. Maisha yako kama yalivyo sasa ni picha ya kile ulichokitengeneza miaka iliyopita. Na maisha yako kwenye miaka ijayo ni picha ya kile unachotengeneza sasa. Maisha yako yaendavyo yanategemea maneno yako.

Jambo la muhimu zaidi kwenye maisha yako ni MANENO yako. Maneno yako yataamua kiwango cha maisha yako duniani, mahusiano yako na Mungu, mahusiano yako na wanadamu, na mahali utakapokwenda milele, mbinguni ama kuzimu. Embu fikiria maandiko yanayotueleza kwamba kuwaombee maadui zetu lakini kuhusu swala la maneno hasi walionena kinyume nasi, biblia inasema hukumu kuwa mkosa. Hauruhusu hilo neno libaki hewani, hapana! Unaliondoa na kutamka uzima.

Maneno yana nguvu sana kiasi kwamba tunaambiwa kwenye maandiko kwamba uzima na mauti upo kwenye nguvu ya ulimi. Kama unaona afya yako ama uweza wako wa kifedha hauendi sawa, tumia maneno yako kuviweka sawa. Wakristo walio kimya hufa kimya. Nena uhai leo!

## UKIRI WA KINABII

**Bwana amefanya maisha yangu kuwa mepesi, ya utukufu na kufurahisha. Ninaishi maisha yasiokuwa na msongo wa mawazo. Niko kwenye pumziko la Mungu hivyo, ninafurahia maisha ya furaha, amani na mafanikio!**

### SOMO LA ZIADA
Isaya 54:17, Mithali 18:21



**Isaya 43:18-19 1 Wakorintho 3:16**
**Hamjui ya kuwa nyie ni hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu?**

Kama unafahamu ya kuwa Roho mtakatifu, ambaye ni muwasilishi wa baraka za Mungu, na vyote tulivyopokea kupitia Yesu Kristo, anaishi ndani yetu, utaishije maisha ya kawaida? Hata kama mwili wako umeumizwa na kuharikiwa na magonjwa na udhaifu, kutafakari hii kweli kutakusaidia mwili wako wote.

Kwenye 2 wakorintho 6:16 anasema kwamba, 'kwa maana sisi ni hekalu la Mungu aliye hai kama Mungu anavyosema, ya kwamba, nitakaa ndani yao, na kati yao nitatembea, nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu.' natamani uone maneno aliyoshagua, 'nitakaa ndani yao' inayomaanisha 'ataishi ndani yao!' hii inamaanisha kwamba ameweka makao makuu ndani yao, na pia anasema nitatembea kati yao.

Sehemu ya huduma ya Roho mtakatifu ndani yako ni kuhakikisha kwamba chochote kinachoenenda tofauti ndani ya mwili wako kinasuluhishwa. Kama unahitaji kufanyika mpya, atakufanya mpya. Tambua kwamba Roho mtakatifu anaishi ndani yako na nguvu zake zote. Unamuhitaji yeye tuu. Uwepo wake ndani yako unakupa ushindi juu ya mipango ya adui na ushawishi mbovu wa dunia hii haleluya!

## UKIRI WA KINABII

Uzima wa milele ni jambo halisi kwangu hata sasa. Ndiyo! Maisha ya ushindi ni yangu. Ninaishi juu ya magonjwa, umaskini, kufeli na kifo, katika jina la Yesu!

### SOMO LA ZIADA

2 Wakorintho 6:16



**1 Yohana 4:4**
**Ninyi, watoto wadogo, mwatokana na Mungu nanyi mmewashinda, kwasababu yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia.**

Mungu hakuridhika na kuwa nami ama kuishi kati yetu, alichagua kuishi ndani ya mioyo yetu. Huo ndio utukufu na uzuri wa ukristo! Ni maisha ya Mungu kupitia wewe. Ni ufunuo wa neno la Mungu kwenye maisha ya mwanadamu!

Maandiko ya leo yanasema mnatokana na Mungu, tafsiri ya kiyunani ni kwamba tumetokea kwa Mungu, mmetengenezwa naye na anaishi ndani yenu. Mpaka hili likawe uelewa wako wa ukristo, ulichonacho ni dini tuu. Kiini cha ukristo, sababu ya kwenda kanisani, kusali, kuubiri injili na kutenda mambo yote tunayotenda sio kwasababu ya dini tuliofuata, bali ni kwasababu tumepokea asili ya Mungu, uhai wake.

Hiki ndicho ambacho Kristo alituletea. Alifanya iwezekane tupokea uzima wa milele. Uhai wa Mungu ambao hauwezi kuharibiwa, wala kutawaliwa. Husiruhusu watu wakurudishe chini, wewe ni wa kimungu na umewashinda! Hakuna chochote kilichosimama kinyume nawe ambacho kinaweza kukuharibu, aliyeko ndani yako ni mkuu kuliko aliyeko ulimwenguni.

## UKIRI WA KINABII

**Ninaishi kwa sheriaya juu zaidi na tofauti, nimetokea juu, nimetengwa kutoka ulimwenguni na kuwekwa kwenye maisha yasiyoharibiwa, katika jina la Yesu haleluya!**

**SOMO LA ZIADA**
1 Yohana 5:11-12



**Wakolosai 3:16**
**Neno la kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, mkifundishana na kuonyana kwa zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu.**

Kama mkristo, ni muhimu sana kuwa na neno la Mungu ndani yako na kutafakari kila wakati. Maandiko yetu ya leo yanatuonesha vile ambavyo neno la Mungu likikaa kwa wingi ndani yetu, misingi ya maisha yako ya kikristo itapatikana ndani ya neno.

Kama ukiamua kupuuzia neno la Mungu, utabaki kwenye kifungo na kuendelea kupitia yale mambo ambayo watu wa dunia hupitia. Neno la Mungu kwenye matendo ya mitume 20, inatuambia kwamba neno la Mungu linakupa urithi wako. Neno la Mungu litakuletea urithi wako. Hii haimaanishi neno linakugawia sehemu yako. Hapana! Ninamaanisha kwamba kupitia neno la Mungu, utaufahamu urithi wako!

Biblia inasema kwamba utaijua kweli na kweli itakuweka huru. Lakini ni kweli ya neno la Mungu na ufunuo ulionao juu ya neno lako ambalo litafanya kazi kwa niamba yako. Hii inamaanisha kwamba unalo jukumu la kuwekeza muda katika neno la Mungu. Chagua neno la Mungu leo na utarudi na shuhuda.

## UKIRI WA KINABII

**Maisha yangu hayajui huzuni, ninapanda juu na kusonga mbele tuu katika jina la Yesu. mapito yangu ni mapito ya haki, hivyo yanang'ara zaidi na zaidi ikikaribia siku kamilifu, haleluyah!**

**SOMO LA ZIADA**
Matendo 20:32, 1 Petro 1:23



**Warumi 4:18**
**Naye aliamini kwa kutarajia yasiyoweza kutarajiwa, ili apate kuwa baba wa mataifa mengi, kama ilivyonenwa, ndivyo utakavyokuwa uzao wako.**

Hadithi ya Ibrahimu na Sara ni mfano bora kwamba hakuna jambo 'lililochelewa sana' kwa Mungu. Neno la leo linasema naye aliamini kwa kutarajia yasiyoweza kutarajiwa, ili apate kuwa baba wa mataifa mengi, kama ilivyonenwa. Alikuwa na miaka mia moja wakati Sara alikuwa na miaka tisini (Mwanzo 17:17).

Yamkini, Mungu alimwambia kwamba atapata mtoto kupitia Sara. ibrahimu aliamini na katika wakati sahihi, Sara alimzaa Isaka. Watu wengine hukata tamaa na kuwaza ni kwanini hawakupata kazi, mikataba, kupandishwa cheo ama pesa mabayo waliombea na kufunga. Hakuna tofauti hata kama hali yako imekosa matumaini kabisa, hakuna jambo 'lililochelewa sana' kwa Mungu.

Muamini kwani yeye ni Mungu awapae wafu uhai, na nayeita vile ambavyo havipo kana kama vimekuwa. Anaishi katika umilele ambao hauna jana wala kesho. Kwake yeye kila kitu ni SASA, na anajidhihirisha kuwa aliyekubuhu kwenye kila hali na haijalishi imekufa kiasi gani, imechelewa ama haiwezekani kwenye macho ya mwanadamu.

## UKIRI WA KINABII

**Ninaweza mambo yote kupitia Kriato anitiaye nguvu, hakuna ambalo litashindikana siku ya leo kwani kwenye mambo yote haya mimi ni zaidi ya mshindi, haleluya.**

**SOMO LA ZIADA**
Mwanzo 17:17



**Yohana 10:10**
**Mwizi haji ila aibe na kuchinja na kuharibu, mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele.**

Japo kuwa Bwana Yesu ni Mungu kikamilifu, alizaliwa mwanadamu kikamilifu. Alipitia majaribu na kuyashinda yote (Waebraniq 4:15). Nguvu hiyo ya kushinda inapatikana kwenye maisha yake. Tena akaweka hayo maisha ndani yako- uhai wa Kristo uko ndani yako.

Leo hii ameketi kwenye mkono wa kuume wa baba, akipumzika baada ya kumaliza kazi, akiwa na sehemu ya mamlaka ya juu zaidi. Na ameweka huo uhai ndani yako, uhai wa Kristo uko ndani yako. Vile ambavyo Yesu yuko, Mungu alipanga ukawe.

Mambo yote bora unayosoma kwenye biblia kuhusu Yesu, hazina zake zote zilizofichwa kwenye agano la kale, na hazina husizoweza kupima zinazopatikana kwenye agano jipya, hayo yote sio kwamba yapo sehemu fulani. Mungu ameweka ndani yako ili ukaishi maisha ya utele ambayo Yesu alikuja kukupatia.

## UKIRI WA KINABII

**Yesu ni mzabibu nami ni tawi, uhai wa Kristo unatembea ndani yangu. Ninatawala kwenye maisha na ni sehemu ya uungu wake haleluya!**

### SOMO LA ZIADA

Waebrania 4:15



**1 Yohana 5:4**
**Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu.**

Unapotenda kwenye imani, haujaribu kujadili juu ya maagizo ya Mungu, unayatenda. Imani haisemi kwamba, 'najua neno la Mungu linasema hivi na hivi lakini tuutazame uhalisia.' imani haiangalii wala kuzingatia uhalisia, inazingatia neno la kulitenda SASA! Imani inayotenda kazi ni ile ambayo haijadili bali huamini neno la Mungu, hulinena na kulitenda.

Tenda neno leo. Imani sio kuruka gizani bali ni kuruka kwenye neno la Mungu. Hivyo ndivyo Ibrahimu alimpata mwanae Isaka (warumi 4:19). Katika upande wa kihalisia, kila kitu kilikuwa kinyume naye kwamba angeweza kuwa baba wa mataifa mengi. Lakini Ibrahimu hakuruhusu huo uhalisia kuharibu imani yake katika neno la Mungu. Alishikilia kwa nguvu neno la Mungu, akiamini kikamilifu kwamba neno la Mungu ni kweli na sio hali za kihalisia.

Hiyo ndiyo kanuni ya imani! Kama ambavyo imani haijali hali za kihalisia, imani haizipuuzii pia! Imani inachofanya ni kukataza huo uhalizia kupata mamlaka ya kuendesha uwepo wako, ikitumainia neno la Mungu kama hakikisho.

Maandiko yetu ya leo yanatueleza kwamba tusikumbuke mambo ya kwanza, sahau yote! Watu wengine huangalia sana yale makosa yao ya zamani, maumivu na maamuzi mabaya na kuvibeba kutoka mwaka mmoja mpaka mwaka mwigine. Hii inakuwa kama mzunguko na unajikuta umekwama kwenye wakati uliopita badala ya kuishi kwenye wakati wa sasa.

Mruhusu Mungu afanye jambo jipya ndani yako kama alivyoahidi kwenye neno lake. Mpatie Mungu nafasi ya kufanya hivyo kwa kurekebisha kilichomo kwenye akili yako. Achilia mambo ya zamani na tengeneza nafasi kwaajili ya mambo mapya. Mafanikio ya wiki hizi 52 zinazofuata inategemea na vile utakavyopanga akili yako.

Tuanze upya, sawa sawa?

## UKIRI WA KINABII

**Woga na kutokuamini havina nafasi ndani yangu, kwani imani yangu kwa Mungu na neno lake ni ushindi ulioshinda dunia! Mimi ni zaidi ya mshindi!**

### SOMO LA ZIADA
2 Wakorintho 4:18



**Yeremia 28:11**
**Maana najua mawazo ninayowawazia ninyi, asema Bwana, ni mawazo ya amani na wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho.**

Sasa, unafanya nini pale ambapo \mungu anakuambia kwamba utakuwa na siku ambazo zimejaa baraka zake siku zako za mbeleni? Unajiandaa! Kabla baraka hazijaja unapanua sehemu ya hema lako pmoja na pazia za hema lako.

Kwa mfano, kama ulikuwa unamuamini Mungu juu ya mtoto, anza kusoma vitabu vya watoto na kuandaa chumba cha mtoto. Jiandae kuwa na mtoto zaidi ya mmoja. Anza kutafuta sehemu kubwa zaidi kwaajili ya familia yako kwani neno la Mungu linasema, 'panua mahali pa hema yako, na wayatandaze mapazia ya maskani yako usiwakataze ongeza urefu wa kamba zako vikaze vigingi vya hema lako.' jiandae kwaajili ya kupanuka.

Kwavile Mungu amekwisha kutamka siku zako za mbeleni kuwa bora, fahamu ya kwamba umesimama kwenye ardhi ya kibali siku ya leo. Tarajia mambo bora kukutokea. Tarajia kuona kibali cha Mungu juu yako na familia yako. Tarajia baraka za Bwana kuongezeka. Tarajia siku nyingi bora kuonekana kwenye maisha yako.

## UKIRI WA KINABII

**Mambo yameenenda vizuri kwangu, mafanikio ni urithi wangu katika jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Wagalatia 3:29



**Yeremia 28:11**
**Maana najua mawazo ninayowawazia ninyi, asema Bwana, ni mawazo ya amani na wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho.**

Sasa, unafanya nini pale ambapo \mungu anakuambia kwamba utakuwa na siku ambazo zimejaa baraka zake siku zako za mbeleni? Unajiandaa! Kabla baraka hazijaja unapanua sehemu ya hema lako pmoja na pazia za hema lako.

Kwa mfano, kama ulikuwa unamuamini Mungu juu ya mtoto, anza kusoma vitabu vya watoto na kuandaa chumba cha mtoto. Jiandae kuwa na mtoto zaidi ya mmoja. Anza kutafuta sehemu kubwa zaidi kwaajili ya familia yako kwani neno la Mungu linasema, 'panua mahali pa hema yako, na wayatandaze mapazia ya maskani yako usiwakataze ongeza urefu wa kamba zako vikaze vigingi vya hema lako.' jiandae kwaajili ya kupanuka.

Kwavile Mungu amekwisha kutamka siku zako za mbeleni kuwa bora, fahamu ya kwamba umesimama kwenye ardhi ya kibali siku ya leo. Tarajia mambo bora kukutokea. Tarajia kuona kibali cha Mungu juu yako na familia yako. Tarajia baraka za Bwana kuongezeka. Tarajia siku nyingi bora kuonekana kwenye maisha yako.

## UKIRI WA KINABII

**Mambo yameenenda vizuri kwangu, mafanikio ni urithi wangu katika jina la Yesu!**

### SOMO LA ZIADA
Wagalatia 3:29



**2 Wakorintho 3:5**
**Si kwamba twatosha sisi wenyewe kufikiri neno lolote kwamba ni letu wenyewe, bali utoshelevu wetu watoka kwa Mungu.**

Wakristo wachache hufahamu kwamba Mungu anaishi ndani yao. Wasingekuwa wanaongea kama wanavyoongea. Hitaji linapojiinua kwenye maisha yao, wengi wanakimbilia kusema 'hapana, siwezi kufanya hilo.' kwanini? Ni kwasababu wanajiamini wao wenyewe, mambo ya kwenye nyama kuwawezesha. Wanajua hawana uwezo ndani yao kufanya jambo hilo.

Lakini unapokuwa na uelewa kwamba Mungu yupo ndani yako, basi unafahamu kwamba uwezo wake ni uwezo wako. Haupewi vikwazo na uwezo wako wa kimwanadamu, na ndiyo maana Paulo alisema, 'ninaweza mambo yote kupitia yeye anitiaye nguvu.'

Haijalishi ni jambo gani unapitia leo, na unaweza kuwa unapitia mambo yasiyowezekana kwenye maisha yako, kiri kwa ujasiri, 'uwezo wangu ni wa Mungu, aliyemkuu zaidi anaishi ndani yangu.' hiyo ni imani inaongea. Na itamuweka mkuu kazini kwaajili yako!

## UKIRI WA KINABII

**Roho wa Mungu anaishi ndani yangu. Uwezo wangu ni wa Mungu na ninaweza mambo yote kupitia yeye anitiaye nguvu, hakuna kinachoshindikana kwangu kwenye huu mwaka wa watu wa kimungu!**

### SOMO LA ZIADA
Wafilipi 4:13



**Yohana 14:27**
**Amani ninawaachieni amani yangu nawapa niwapavyo mimi sio kama ulimwengu utoavyo. Msifadhaike mioyoni mwenu, wala msiwe na woga.**

Ule usiku kabla Yesu hajafariki, aliwapa mitume wake amani, " amani yangu nanawaachieni, amani yangu nawapa..." hii amani haikuwa na mitume pekee bali ni yetu pia. Tunayo amani yake.

Unapomuamini Yesu Kristo, yeye ambaye ni mfalme wa amani anakuja kukaa ndani yako. Na kama mfalme wa amani yu ndani yako, kila baraka unayohitaji ambayo inahusu utulivu na uzima iko tayari ndani yako.

Mawazo na wasiwasi unapokujia, jikumbushe maneno haya, 'msifadhaike mioyoni mwenu, wala msiwe na woga.' hata mambo yanapoonekana mabaya sana, sema hivi, "Bwana nakataa kuwan na wasiwasi juu ya swala hili, katikati ya haya yote, ninaona kazi kamilifu ya Kristo. Alisema imekwisha! Hivyo basi, uponyaji wa mwanangu umefanyika. Ndoa yangu imebarikiwa. Madeni yangu yameondolewa. Sitoruhusu moyo wangu usumbuliwe na haya."

## UKIRI WA KINABII

**Nimebarikiwa kupita kipimo. Mimi ni kama mti uliopandwa pembeni ya mito ya maji. Kila ninachofanya kinafanikiwa katika jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Zaburi 1:1-4



**Yoshua 1:8**
**Kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako, bali tafakari maneno yake mchana na usiku, upate kuangalia kutenda sawasawa na maneno yote yalioandikwa humo maana ndipo utakapofanikisha njia yako, kisha ndipo utakapositawi sana.**

Kufaulu ama kufeli sio ajali. Yoshua aliambiwa kwamba kama akikaa ndani ya neno, atafanikisha njia yake. Mungu hakuwa mwenye jukumu la kufanikiwa kwake. Alipewa chaguo la kufanikiwa ama kutokufanikiwa.

Kama unafanya kanuni za mafanikio kulingana na neno la Mungu, unao uhakika wa kupata mafanikio katika kila eneo la maisha yako. Kwenye mkono mwingine, anayeishi bila malengo, kusudi wala kuelewa njia yake, atafeli sana kwenye maisha yake. Bado ni mwanzo wa mwaka, wakati mzuri wa wewe kupanga mikakati kwa Roho na kushinda. Kumbuka kwamba haitoshi kutumainia mafanikio, fanya yatokee. Ni changuo ambalo lazima ufanye.

Tumia neno la Mungu kuyachora maisha yako, kama ambavyo Yoshua alifanya, tengeneza njia yako ya mafanikio. Tazama maandiko yetu ya leo yanasema kwamba utafanikisha njia zako. Hii inaweka jukumu la mafanikio yako kwenye mabega yako. Nena kupandishwa kwako, ushindi ni wako!

## UKIRI WA KINABII

**Siwezi kushindwa kwenye haya maisha, ninaye mpanga mipango wa ajabu pamoja nami, siwezi kushindwa. Ninashinda hivi leo katika jina la Yesu!**

### SOMO LA ZIADA
Warumi 8:37



**Warumi 4:13**
**Kwa maana ahadi ile ya kwamba atakuwa mrithi wa ulimwengu alipewa Ibrahimu na uzao wake, si kwa sheria bali kwa haki aliyohesabiwa kwa imani.**

Mungu alimuahidi Ibrahimu kwamba atakuwa mrithi wa ulimwengu. Basi husiwe na haraka kusema kwamba hii ahadi ilikuwa ya Ibrahimu na sio yako. Andiko linasema, 'kwa maana ahadi ile ya kwamba utakuwa mrithi wa ulimwengu alipewa Ibrahimu na uzao wake, si kwa sheria bali kwa haki aliyohesabiwa kwa imani.' hivyo basi, ahadi haikuwa kwa Ibrahimu bali kwa uzao wake, yaani mimi nawewe ambao ni wa Kristo. 'Na kama ninyi ni wa Kristo, basi mmekuwa uzao wa Ibrahimu, na warithi sawasawa na ahadi (wagalatia 3:29).'

Zingatia kwamba Mungu hakusema kwamba utakuwa mrithi wa nchi unayoishi bali mrithi wa ulimwengu wote! Neno ulimwengu hapa ni neno la kiyunani 'kosmos' lenye maana ya dunia pamoja na yote mema yaliopo humo. Haya yote ni urithi wako kupitia haki inayohesabiwa kwa imani ndani ya Yesu na kazi yake timilifu msalabani. Unapokea haki hii kutoka kwa Mungu kama zawadi, hivyo hauhitaji kuipata kwa matendo.

Husiwasikilize wale wanaokuambia kwamba utapata nafasi ya kufurahia baraka hizi ufikapo mbinguni. Kwanini uhitaji utajiri mbinguni? Huko hata njia zimetengenezwa kwa dhahabu, (tazama; Ufunuo 21:21). Tena kwanini uhitaji uponyaji mbinguni? Hakuna magonjwa huko. Hivyo unahitaji afya na mahitaji hapa na sasa. Sikilia urithi wako hivi leo. Yesu alilipia kwa damu yake. Husiache zikakupita.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni uzao wa Ibrahimu, na kwasababu hiyo, mimi ni mmiliki wa vyote. Mafanikio ni yangu katika jina la Yesu, sitapungukiwa na kitu.**

**SOMO LA ZIADA**
Wagalatia 3:29



**Wafilipi 3:13**
**Ndugu, sijidhanii nafsi yangu ya kwamba nimekwisha kushika ila natenda neno moja tu nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachichumilia yaliyo mbele.**

Kujuta juu ya mambo ya nyuma na kuwa na wasi wasi na mambo yajayo haisaidii kitu. Mtazamie Baba yako wa mbinguni. Yeye ni wako hata sasa na unaweza kuwa na hakika kwamba atakusaidia mahitaji yako.

Hii ndiyo sababu katika maandiko yetu ya leo, mtume Paulo anatuambia kusahau yaliyonyuma na kuyachichumia yaliyo mbele. Mahali hapa alikuwa anatuma siri ya mafanikio yake, kumbuka alikuwa muuaji aliyebadilika na kufikia hatua ya kuandika vitabu 14 vya agano jipya. Acha kuishi kwenye maisha yako ya zamani, Mungu anao mpango kwa ajili yako na haijalishi ni kitu gani ulipitia huko nyuma, atatengeneza uzuri kutoka majivuni.

mungu alimtuma mwanae kufa kwaajili yako! Yesu alikununulia maisha ya utele na yenye kusudi kupitia damu yake! Alikununulia haki ya kutembea kwenye afya ya kiungu siku zote za maisha yako! Alikupa haki ya utoaji wake hata pale ambapo uchumi unaanguka! Husiruhusu makosa ya nyuma kukurudisha nyuma kwani siku za usoni ni zako!

## UKIRI WA KINABII

**Ninatembea kwa ujasiri na bila uwoga, nikijawa imani na ujasiri. Nimelindwa kiungu kutoka kwenye nguvu zote za giza na ni mshindi ndani ya Kristo. Maisha yangu ni ya utukufu na ukamilifu haleluya!**

### SOMO LA ZIADA
Yeremia 29:11

OSBORN INSTITUTE of THEOLOGY



CERTIFICATE / DIPLOMA

1ST SEMESTER STARTS
1 MARCH 2021

# ENROLMENT NOW OPEN

THE OSBORN INSTITUTE OF THEOLOGY FOUNDED BY PROPHET UEBERT ANGEL AND FULLY ACCREDITED BY TRANSWORLD ACCREDITING COMMISSION INTERNATIONAL, PROVIDES AN AWARD-WINNING ONLINE LEARNING PLATFORM THAT EQUIPS MEN AND WOMEN WITH THE REVEALED WORD OF GOD. OIT PREPARES MEN AND WOMEN TO SHARE AND BEAR WITNESS OF JESUS CHRIST TO THE CHURCH AND THE WORLD.

ENROL NOW AT WWW.OSBORNINSTITUTE.COM


LEARN HOW TO BE A
MILLIONAIRE
MILLIONAIRE
ACADEMY
WITH UEBERT ANGEL
REGISTER NOW AT
WWW.THEMILLIONAIREACADEMY.ORG



**2 Wakorintho 3:18**
**Lakini sisi sote, kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano huo huo, toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa utukufu utokao kwa Bwana, aliye Roho.**

Ukiangalia kwenye kioo unamuona nani? Ndiyo, unajiona wewe mwenyewe. Ila Mungu hataki ujione wewe katika hali ya mwili. Anataka uone uhalisia wako ndani ya Kristo. Unaweza kuwa mgonjwa, mdhaifu, masikini na mwenye msongo wa mawazo, lakini Mungu anataki ujione vile ambavyo yeye anakuone, uliyepona, mwenye nguvu, mwenye kibali, na mkamilifu kwasababu Kristo yuko ndani yako (Wakolosai 1:27).

Mungu anataka uone utukufu wa mwanae aliyeko ndani yako kupitia Roho wake. Ufanyapo hili, neno lake linasema kwamba unatoka utukufu hadi utukufu. Unatoka kwenye kuwa mgonjwa mpaka kuwa aliyepona, kutoka kuwa aliyeshindwa na kuwa aliyeshinda, haleluya! Unabadilishwa kuwa mfano huo.

Siku ya leo unapotafakari neno la Mungu, unaona utukufu wa Bwana ambaye ndiye mwenye afya ndani ya mwili wako dhaifu, unabadilishwa kutoka kwenye ugonjwa hadi kupona. Hili haliwezekani kwa nguvu zako mwenyewe, kwa kula vizuri ama kufanya mazoezi bali ni kwa Roho wa Bwana. Unapoona zaidi ndivyo unavyobadilika hata zaidi, mpaka unakuwa kile unachoona.

## UKIRI WA KINABII

**Neno la Mungu lipo moyoni mwangu na mdomoni mwangu likitengeneza matokeo. Natembea kwenye amani, mafanikio, afya ya kiungu, ulinzi, nasonga mbele na kutembea kwenye baraka za kiungu leo na hata milele, haleluya!**

**SOMO LA ZIADA**
Waebrania 4:12



**2 wakorintho 5:20**
**Basi tu wajumbe kwa ajili ya Kristo, kana kwamba Mungu anasihi kwa vinywa vyenu twawaomba ninyi kwaajili ya Kristo mpatanishwe na Mungu.**

Ni jambo moja kujua wewe ni nani na jingine kujua wewe ni wa nani. Mwaka huu umetamkwa kuwa mwaka wa watu wa kimungu lakini unaleta maana kwa wale tuu ambao wanajua wao ni nani. Maandiko yetu ya leo yanasema kwamba sisi ni wajumbe wa Kriato, hilo peke yake latosha kunipeleka kwenye haleluya!

Kuwa mjumbe unapewa haki kamili ya ufalme unaowakilisha na haki ya kufata sheria za ufalme unaotokea hata kwenye nchi ya kigeni. Hiii ndio maana ubalozi wa Marekani utapepea bendela yao Irani bila kikwazo.

Hivi leo haijalishi uchumi wa ncho yako ukoje ama ni watu wangapi wanasimamishwa kazi. Wewe ni mjumbe wa Kristo na kama kuna uteshelezi kwenye ufalme wa Mungu, utakuwa salama. Umepewa nguvu ya kwenda na kutawala maeneo yote ya maisha kwa sababu ya nafasi yako ndani ya Kristo.

## UKIRI WA KINABII

**Ninaye Kristo ndani yangu, tumaini la utukufu, nakataa kuwa mtumwa wa mambo ya maisha haya na ninabeba mamlaka yote ya ufalme wa Mungu, haleluya!**

**SOMO LA ZIADA**
1 Yohana 4:4



**Zaburi 65:11**
**Umeuvika mwaka taji ya wema wako, Mapito yako yadondoza unono.**

Wanauchumi wanaweza wakawa wamechora picha ya uchumi, lakini kwenye upande wa Mungu, yeye ameuvika mwaka wema na unono! Utoshelevu wa Mungu haujali matukio ya ulimwengu. Kwahiyo kwenye wakati mzuri ama mbaya, tarajia kila mwezi, wiki na siku kuzungukwa na wema wake. Tegemea unono kwenye kila hitaji lako.

Sasa, ukiangalia kwa karibu neno lililotafsiriwa 'unono' kwa kiyunani ni neno 'deshen' lenye maana ya unene. Wazo kuu hapa ni kwamba kuna utoshelezi, baraka na uzazi. Hivyo, kama ulikuwa unamwamini Mungu kwaajili ya mtoto, amini kwamba mwaka huu utapata ujauzito.

Umebarikiwa na sio kwasababu ya mwonekano wako, matendo yako, vigezo vyako, wala uzoefu wako bali ni kwasababu ya kazi ya Kristo iliyomalizika. Yeye peke yake amekustahilisha kupokea taji ya wema na unono maisha yako yote!

## UKIRI WA KINABII

**Natembea kwenye baraka za Mungu. Maisha yangu hayajui maumivu, ninapanda juu naninkwenda mbele tuu katika jina la Yesu. mapito yangu ni mapito ya haki na hivyo yanang'ara zaidi na zaidi mpaka siku ya ukamilifu, katika jina la Yesu.**

### SOMO LA ZIADA
Zaburi 23

## Jibu lako liko ndani yako.



**Mwanzo 2:22**
**Na ule ubavu alioutwaa katika Adamu Bwana Mungu akaufanya mwanamke, akamleta kwa Adamu.**

Ukweli mmoja unaouma sana ni kuambiwa kwamba yote unayohitaji yako ndani yako. Unaweza ukawa unalalamika kuhusu fedha, afya na mahusiano lakini suluisho liko ndani yako.

Unatembea na majibu yako na yale ya familia yako. Tazama, Adamu alikuwa peke yake mpaka Mungu aliona sio vema kwa Adamu kuwa peke yake lakini mwenzi wake alikuwa ndani yake. Majibu ya Adamu hayakutoka nje bali ndani yake. Unaweza kuwa kama Adamu ukitafuta pesa, biashara, fursa ambazo tayari zimewekwa ndani yako. Siku ya leo tambua kwamba unayo majibu.

Pesa yako, afya yako na miradi yako iko ndani yako. Siku ya leo unapotazama kioo cha neno la Mungu, unaona majibu kuhusu biashara yako ndani yako, kwani biblia inasema kwamba Kristo ni hekima yako. Unajua ni nini cha kufanya na ni wakati gani sahihi wa kukifanya. Ndugu zangu, mambo yote ni yenu ndani ya Kristo, huu sio muda wa kulia bali tazama kwenye kioo cha neno la Mungu na tambua alichokutendea!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mbeba suluhisho na kila jibu ninalohitaji kwenye haya maisha yako ndani yangu. Nachagua kuacha kulalamika, bali kuingia ndani yangu na kupata majawabu.**

**SOMO LA ZIADA**
2 Wakorintho 3:18



**Luka 1:37**
**Kwa kuwa hakuna neno lisilowezekana kwa Mungu.**

Andiko letu la hapo juu ni andiko ambalo linanenwa na watu wengi lakini wengi hawafahamu nguvu iliyopo ndani ya andiko hili. Mungu hataki uendelee kugonga milango ambayo imeshafungwa. Anataka uwe kwenye eneo la mambo yawezekanayo sasiopimika.

Hii ndiyo sababu Mtume Paulo aliweza kusema kwamba "ninaweza yote kupitia yeye anitiaye nguvu." ndugu zangu ukiwa umezaliwa upya, upo ndani ya Kristo na Kristo hawezi kufeli, hawezi kushindwa na hawezi kuwa tasa. Haufanyi kazi kulingana na nguvu za kibinadamu bali ni kwa uwezo wa Roho mtakatifu anaeishi ndani yako.

Wewe ni mtu mpya ndani ya Kristo, mkubwa kuliko shetani na majini, ni wakati wa kuingia ndani ya neno na kutambua ambacho ni chako. Umeingia kwenye sehemu ya uwezo husiokuwa na kikomo, na hivyo kama mwana wa Mungu hakuna jambo amabalo litakuwa gumu kwako. Nedna kafanye mambo ambayo ulishindwa kufanya ama mambo yaliyoonekana kama hayawezekani, utarudi na shuhuda.

## UKIRI WA KINABII

**Kuanzia leo, hakuna jambo litakaloshindikana kwenye maisha yangu, ninayo nguvu na neema ya kutosha kufanya jambo lolote katika jina la Yesu!**

### SOMO LA ZIADA
Wafilipi 4:13



**2 Wakorintho 4:13**
**Lakini kwa kuwa tuna roho ile ile ya imani kama ilivyoandikwa, naliamini, na kwa sababu hiyo twanena.**

Bwana Yesu alionesha kuwa juu ya mazingira ya maisha yake kwenye huduma yake ya mwanzo. Kuna wakati aliufata mti wa tini akitarajia kupata chakula lakini mti huu haukuwa na matunda kwani haikuwa msimu wake wa kuzaa matunda. Biblia inasema Yesu aliuwambia mti kwamba, "tangu leo hata milele mtu asile matunda kwako"

Tazama alichowaambia wanafunzi wake baada ya wao kuona mti umenyauka, " amin, nawaambia, yeyote atakaeuambia mlima huu, ng'oka ukatupwe baharini, wala asione shaka moyoni mwake, ila aamini kwamba hayo asemayo yametokea, yatakuwa yake (Marko 11:23)."

Hapa Yesu hakuwa anaongea kwa mafumbo kama ambavyo watum wengi hudhania. Kumbuka kwamba kwenye andiko lililopita aliongelesha mti! Alikuwa anatuonesha nguvu na uweza wa maneno yetu na alituhakikishia mara nyingi tofauti. Maneno yako yaliojaa imani yanaamua ubora wa maisha yako! Haijalishi umejikuta kwenye hali ya namna gani, unaweza kuleta mabadiliko kwa maneno yaliyojaa imani!

## UKIRI WA KINABII

**Nitatamka na kukiri uponyaji wa kiungu kwenye mwili wangu, kila dalili inaniondoka katika jina la Yesu, ninaamuru huo uvimbe kupotea katika jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Marko 11:23



**1 Wakorintho 14:2**
**Maana yeye anenaye kwa lugha, hasemi na watu, bali husema na Mungu maana hakuna asikiaye lakini anena mambo ya siri katika roho yake.**

Mwaka 1942 wamarekani waliweza kushinda vita dhidi ya wajapani kwa kutumia lugha ya siri kutoka kwa watu wa Najavo, ambapo neno la Najavo lilisimamia maneno muhimu na mbinu ya kivita. Wamarekani waliweza kuwasiliana baina yao kuhusu mipango yao ya kumpiga adui bila adui kuweza kuelewa. Wamarekani walikuwa wanaongea siri. Ni furaha ya namna gani kujua ya kuwa unaweza kunena siri?

Ndugu zangu hili ndilo unalofanya ukiwa unanena kwa lugha. Unasema siri zisizoweza kufichuka ambazo adui hawezi kutafsiri. Kwa uelewa wako binafsi unaweza husielewe lakini roho yako inaelewa vizuri na mambo yanaanza kubadilika kwenye maisha yako na kujipanga na mipango ya Mungu kwenye maisha yako.

Unashusha mikakati na kunena maneno yanayorekebisha hali za maisha yako. Unajijenga kwa kunena siri ambazo adui na ulimwengu hauwezi kutambua. Unaponena kwa lugha siku ya leo, unanenasababisha mabadiliko kwenye ulimwengu wa roho na hakuna kinachoweza kukuzuiya!

## UKIRI WA KINABII

**Ninavyonena siri za rohoni, maisha yangu yanakuwa mazuri na ninasababishwa kufanikiwa katika jina la Yesu, haleluyah!**

**SOMO LA ZIADA**
Yuda 20



**1 Petro 1:23**
**Kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili si kwa mbegu iharibikayi, bali kwa ile isiyoharibika kwa neno la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele.**

Kwenye biologia kuwa makundi mbalimbali ya uhai ikiwemo uhai wa miti na uhai wa wanyama. Je, wajua ya kwamba kuna uhai ambao ni zaidi ya huu uhai wa kibiologia? ni uhai wa kiroho,nuhai wa kimungu.

Wewe ni mzawa wa Mungu, umetokana nae na ni mbegu yake. Yeye ni baba yako kweli. Chanzo chako ni Mungu. Kile kinachomfanya Mungu ndichokinachotembea kwenye mishipa yako. Umeundwa kwa neno. Umezaliwa kwa neno. Umefanyika kwa neno.

Kila kitu kuhusu maisha yako ni neno na kipo kwasababu ya neno na hii ndio sababu unahitaji neno. Neno ni maisha yako.

Alikuumba kuwa na mamlaka na kutawala maishani na unaweza kufanya hivi kupitia neno. Alikuumba kuwa bwana kwenye maisha yako lakini haya yawezekana kupitia neno. Haya ni maisha kama alivyonayo Mungu, katika ubora wake bila kuwako kilichoharibika wala kinachokosekana.

## UKIRI WA KINABII

**Nimejawa neno. Maisha yangu yamefanikiwa maana ameniweka juu ya kila hali katika jina la Yesu!**

### SOMO LA ZIADA
Wakolosai 3:3-4

# Unachosema ndicho unachopata



**Mithali 18:20-21**
**Tumbo la mtu litajazwa matunda ya kinywa chake atashiba maneno ya midomo yake. Mauti na uzima huwa katika uwezo wa ulimi na wao waupendao watakula matunda yake.**

Maneno tunenayo yanaunda maisha yetu. Maisha yako ni ujumla wa maneno unayonena kwa midomo yako. Hili limedhibitishwa kisayansi. Majaribio yalifanywa na wanasayansi kwa mabeseni mawili ya maji yaliyoganda. Beseni la kwanza lilipigiwa mziki mzuri na kunenewa maneno mazuri na beseni la bili lilipigiwa mziki mbaya na kunenewa maneno ya hasira. Hiki kilifanywa kwa siku kadhaa n baada ya hapo, lile beseni lililokuwa likinenewa maneno mema lilianza kutengeneza michoro mizuri katika barafu zilizokuwa zikiganda, kwa upande mwingine, lile beseni lenye kunenewa mabaya lilianza kutengeneza michoro mibaya ya barafu.

Mwili wako umeundwa kwa asilimia 60 ya maji, je unaweza kuwaza kitatokea nini kama ukianza kunena mambo hasi? Ndio maana watu wengi wanaumwa. Maandiko yetu yanasema uhai na mauti yako kwenye nguvu ya ulimi. Unaweza kuchagua siku ya leo kunena mambo sahihi kwenye maisha yako na kuanza kuishi maisha unayotaka, ama unaweza kuchagua kutamka maneno hasi na kuanza kuishi maisha mabovu kulingana na kile ambacho maneno yako yanaweza kutengeneza. Biblia inatupa chaguo, ni juu yako.

Ndugu zangu unaweza kuchagua kuwa nabii wa maisha yako kwa kunena neno la mungu katika maisha yako juu ya kila hali na ukaone ndoto zako na matamanio yako yakitimia. Chagua uhai!

## UKIRI WA KINABII

**Maneno yangu yamebeba nguvu ya kusababisha mabadiliko kwenye kila eneo la maisha yangu. Siku ya leo nachagua kunena uhai na kuona udhihirisho wa ndoto zangu katika jina la Yesu, haleluya!**

**SOMO LA ZIADA**
Yohana 6:63



**Wafilipi 2:10**
**Ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi.**

Tunayo silaha kuu zaidi upande wetu, Bwana ametupa kibali cha kimahakama cha kutumia jina lake kwenye mambo yetu. Kila mwamini anaweza kutumia jina lake kurudisha mambo yake kwenye mstari. Jina la Yesu lina nguvu kama Yesu mwenyewe.

Unapoomba katika jina la Yesu ni kama kwamba Yesu mwenyewe amesimama na maneno unayonena yanatoka kwenye mdomo wake. Yanabeba kibali sawasawa na kama Yesu angenena. Pata picha kama ukiiamuru hiyo kansa kuondoka ama hayo marumbano kwenye ndoa yako kubadilika na kuwa mani kupitia hili jina bora.

Maandiko yetu ya leo ynasema kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, inamaana hakuna anayeweza kukupinga inapokuja kwenye hili jina. Unayo nguvu ya kusababisha mabadiliko kwenye maisha yako, chukuwa kibali katika jina la Yesu na uone kila jambo likikaa sawa kwenye maisha yako.

## UKIRI WA KINABII

**Hivi leo, mimi nachukuwa mamlaka ya kifedha juu yangu, naamuru kila aina ya ugonjwa kuuacha mwili wangu, natamkia amani kwenye kila dhoruba maishani mwangu.**

**SOMO LA ZIADA**
Marko 16:17



**Warumi 1:16**
**Kwa maana siionei haya injili kwasababu ni uweza wa Munguuuletao wokovu, kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia.**

Kama mwana wa Mungu lazima uwe na chachu ya kusambaza injili, lazime utamani ndani yako kupeleka injili kwa waliopotea. Wewe ni mlezi wa injili. Hivyo basi, ni wajibu wako wa kiungu kuipeleka ulimwenguni.

Utakapoelewa kwamba Yesu ndiye njia pekee, utasimama kwaajili ya injili. Tia mafuta chachu yako ya injili. Endelea kuhubiri na kuwaeleza watu juu ya habri njema ya neema ya Mungu. Zungumza juu ya injili pamoja na wale wanaopenda injili na waombee wale ambao bado hawajasikia neno la wokovu.

Unao wajibu wa kutangaza habari njema, sio kwa maneno yako tuu bali hata namna unavyojibeba. Paulo alisema, nimeitwa kumdhihisha mwanae aliyeko ndani yangu, kwa lugha nyingine, ulipofanya biashara zake, na alipocheza michezo \kristo alidhihirika ndani yake. Huu ni wito wa kila mkristo n sio Wachuganji na walimu, ni wakati wa kujibu huu wito.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mji uliojengwa mlimani, siwezi kufichika, Mungu amenifanya ishara na maajabu kwenye hiki kizazi na ninavuna nafsi kwani ufalme wa Mungu unadhihirika kupitia mimi haleluya!**

### SOMO LA ZIADA
Wagalatia 1:16



**Waefeso 5:18**
**Tena msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ufisadi bali mjazwe Roho. Mkisemezana kwa zaburi na tenzi nyimbo za rohoni, huku mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu.**

Furaha ni matokeo ya Roho ya mwanadamu iliyoundwa upya. Hivyo, kila mkristo anatakiwa kuhisi furaha ya Bwana na kuhidhihirisha wakati wote. Furaha ya Bwana maishani mwako inatakiwa kuwa huru kutoka kwenye hali zako za maisha. Haijalishi ni hali gani, ama tukio litakalotaka kukufanya ukose furaha lakini unaweza kuwa na furaha ndani ya Roho mtakatifu.

Maandiko yetu ya leo yanatueleza namna ya kubaki kwenye furaha, kujazwa na Roho. jifunze kujiongelesha kwa zaburi na tenzi pamoja na nyimbo za rohoni. Kuwa na mwimbo wa bwana moyoni mwako siku zote! Kwa namna hiyo, unabaki ukiwa umejazwa furaha, na unasababisha ndani yako na kwenye mazingira yaliyokuzunguka hali ya furaha.

Unavyoendelea kushiriki rohoni, maisha yako yatajawa na furaha pamoja na mafanikio. Itakuwa ngumu sana kwa jambo lolote kukosesha furaha moyoni mwako. Hivyo, hivi leo furahini katika roho kwani furaha ya Bwana ni nguvu yenu. Haleluya!

## UKIRI WA KINABII

**Bwana, ninakushukuru kwa neno lako ninavyolitafakari na kurikiri kila mara. Linafanya kazi mwilini mwangu kama dawa. Neno lako li hai, tena lina nguvu. Tena lina ukali kuliko panga uwao wote ukatao kuwili. Linauwisha mwili wangu na kuupatia nguvu. Bwana atukuzwe!**

### SOMO LA ZIADA
Wafilipi 4:4



**Yakobo 4:6**
**Lakini hutujalia sisi neema iliyozidi kwa hiyo husema, Mungu huwapinga wajikuzao, bali huwapa neema wanyenyekevu.**

Kwenye ulimwengu wa rohoni, Mungu ameamua neema yake kutiririka chini ambapo wale walioamua kujishusha hukuta neema ya Mungu ikifanya kazi kwao.

Neno la kiyunani ambalo limetumika kama unyenyekevu mahali hapa ni nenotapeinos lenye maaana ya kulala ama mwenye kipimo cha chini. Hivyo Mungu hajafanya neema hii kuwepo kwaajili ya wale wanaojiinua bali wale wanaojiweka chini ndio wanaopata kutembea kwenye hii neema.

Katika hatua hii maisha ni matamu, utaishi kwenye nyumba ambayo hukujenga, inaonekana kana kwamba maisha yanakupa mambo bila kufanya jambo lolote.

Lakini kumbuka kwamba, kufikia hatua hii ya neema unatakiwa kujishusha, husiruhusu kiburi kikakukosesha neema hii. Jishushe nae atakuinua, haleluya!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni wakimungu, nachagua kujishusha katika kila jambo ninalotenda hivi leo, ninacho kibali kikuu na neema ya Mungu itanifanikisha katika jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Yakobo 4:10


TheGoodNewsWorld Helplines
USA: +1 (240) 781-6942
UK: +44 333 344 8612
RSA: +27 (51) 004-0209
www.goodnewsworld.com



# HAVE YOU RECEIVED JESUS CHRIST YET?

WE INVITE YOU TO MAKE JESUS CHRIST THE LORD OF YOUR LIFE BY PRAYING THIS PRAYER;

"O LORD GOD, I COME TO YOU IN THE NAME OF JESUS CHRIST. I BELIEVE WITH ALL MY HEART IN JESUS CHRIST, SON OF THE LIVING GOD. I BELIEVE HE DIED FOR ME AND GOD RAISED HIM FROM THE DEAD. I BELIEVE HE'S ALIVE TODAY. I CONFESS WITH MY MOUTH THAT JESUS CHRIST IS THE LORD OF MY LIFE FROM THIS DAY. THROUGH HIM AND IN HIS NAME, I HAVE ETERNAL LIFE; I'M BORN AGAIN. THANK YOU LORD, FOR SAVING MY SOUL! I'M NOW A CHILD OF GOD. HALLELUIAH!"

CONGRATULATIONS! YOU ARE NOW A CHILD OF GOD.

TO RECEIVE MORE INFORMATION ON HOW YOU CAN GROW AS A CHRISTIAN, PLEASE GET IN TOUCH WITH US ON


UK: +44 3333 448 612

USA +1 240 781 6942

RSA +27 51 004 0209

# SCRIPTURE PASSAGE FOR PROTECTION

## ISAIAH 54:

14 I AM BUILD SOLID, GROUNDED IN RIGHTEOUSNESS,
FAR FROM ANY TROUBLE—NOTHING TO FEAR!
FAR FROM TERROR—IT WON'T EVEN COME CLOSE!

15 IF ANYONE ATTACKS ME,
I WILL NOT THINK FOR A MOMENT THAT GOD SENT THEM,
AND IF ANY SHOULD ATTACK ME,
NOTHING WILL COME OF IT.

16 GOD CREATED THE BLACKSMITH
WHO FIRES UP HIS FORGE
AND MAKES A WEAPON DESIGNED TO KILL.
HE ALSO CREATED THE DESTROYER—

17 BUT NO WEAPON THAT CAN HURT ME
HAS EVER BEEN FORGED.
ANYONE WHO ACCUSES ME
WILL BE DISMISSED AS A LIAR.
I AM GOD'S SERVANT SO THIS IS WHAT I CAN EXPECT
GOD WILL SEE TO IT THAT EVERYTHING
WORKS OUT FOR THE BEST FOR ME."

THIS IS WHAT GOD SAYS TO ME AND IT WILL NOT FAIL IN JESUS'S NAME!